Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Kwa hakika Allah Anaamuru uadilifu, na hisani, na kuwapa (watu kama uwapavyo) ndugu; na Anakataza upujufu, na uovu, na uasi. Anawanasihini ili mpate kufahamu. (16:91)

JUZU 77 No. 193 | JUM II - RAJAB 1439 AH | MACHI/APRIL 2018 | AMN./SHAHD. 1397 HS | BEI TSH. 500/=

Khalifatul Masih V a.t.b.a awaambia Waaminio

Ustawi Umo Katika Khulka Njema

Katika Hotuba ya Sala ya Ijumaa ya tarehe 02/03/2018, Hadhrat Hadhrat Amir-ul Muminiin aliwakumbusha Waaminio juu ya Kujitahidi katika Wema, Khulka Njema na Mwenendo Nzuri.

Baada ya Tashahhud, Taawwudh na Surat Faatihah, Hadhrat Amir-ul Muminiin (a.t.b.a) alisema: Dini tukufu ya Islam, jinsi ilivyotoa mafundisho ya kuonesha khulka zilizotukuka bila kuacha sehemu yoyote na kuzionesha kila khulka kwenye mahala pake, nyumbani na katika jamii, hakuna dini nyingine yoyote iliyoeleza kwa namna hii.

Lakini kwa bahati mbaya ni Waislam tu ambao wako chini kidaraja hili (la khulka). Wasio Waislam wanawanyooshea vidole kwa sababu matendo yao ni tofauti na mafundisho yao. Mtume wetu mtukufu s.a.w. aliwatilia mkazo mara kwa mara watu wake, hasa kwa matendo yake kwa ajili ya kujipatia viwango vya juu vya khulka.



Sehemu ya waumini ndani ya Baitul Futuh, msikiti uliopo jijini London ambao Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a. hutoa hotuba zake za Ijumaa na kurushwa duniani kote kwa njia ya satelaiti.

Lakini wana madai tu ya kumpenda Mtume s.a.w., ndiyo maana Mwenyezi Mungu Alimtuma Masihi Aliyeahidiwa as lakini hawaelekei huko bali wameruka mipaka katika upinzani wao katika baadhi ya maeneo, na kinyume cha khulka nzuri, wanatumia lugha chafu kuliko yule aliyechafuka zaidi na wanaendelea kupata matokeo (adhabu) yake pia.

Hali yao hii, inatuelekeza sisi Waahmadiyya kwamba tujipatie khulka nzuri kwa juhudi zetu zote. Tujifunze tabia zote nzuri zinazoendana na mifano ya Mtume s.a.w. na mafundisho yake, vinginevyo

Endelea uk 3

Namna ya kuepusha Migogoro na kujenga Mahaba Katika Ndoa

Na Yuusuf Mgeleka, Kahama

Khutba iliyoandaliwa na kuwasilishwa kwenye Semina ya Wanandoa tarehe 04 Machi 2018, Kitonga jijini Dar.

'Na kama mke akiogopa kwa mume wake kugombanagombana na kutengana tengana, basi si vibaya kujirekebisha kwa kufanya suluhu, maana suluhu ni bora. Na ubakhili umewekwa ndani ya nafsi, lakini kama mkifanya hisani na kushika ucha Mungu, basi bila shaka Allah anazo habari za mnayoyatenda.' (Surah An-Nisaa Aya ya 129)

Ndugu zangu wapendwa, wanandoa.

Assalaam alaikhum warahmatullah wabarakatuh.

Hadhrat Khalifatul Masih wa 5 a.t.b.a. aliwahi kutoa khutba ya Ijumaa tarehe 19.5.2017 na alieleza kuwa: Ndani ya ndoa



huwepo na hali ndogondogo za misukosuko ya hapa na pale kwa wanandoa, ambapo alifafanua kuwa iwapo changamoto hizo ndogondogo hazitarekebishwa ndio hupelekea mazingira ya kugombana gombana. Sura niliyoisoma hapo mwanzo kabisa inaonyesha juu ya njia sahihi ambazo tunaweza kutumia katika kuweka sawa ndoa zetu.

Hapa Hudhuur anwar (a.t.b.a) anatuasa ya kwamba hali hizi ndogondogo za mke na mume zitokeapo na kupelekea kuanza kutofautiana, kwanza hupaswa kurekebishwa haraka sana na wanandoa wenyewe kwa

Endelea uk 7

JE WAJUA?

Soka Lilianzaje?

Na Mwl Adullah H Mbanga

Mpira wa miguu, Mchezo uliofanikiwa kuteka hisia za watu wengi kuliko mchezo wowote duniani. Ni mchezo ulioteka mioyo ya watu wa jinsia, rika na haiba tofauti. Ni mchezo ambao Aghalabu huchezwa kila siku katika maeneo mengi zaidi duniani.

Soka, kandand, kabumbu, gozi, kipute n.k yote ni baadhi ya majina yanayoweza kutumika kuwakilisha mchezo huu pendwa ulioanzwa kwa ridhaa na hatimaye kugeuka kuwa biashara kubwa kuliko zote duniani. Mpira wa miguu umejijengea haiba kubwa katika Nyanja za kijami, kisiasa na kitamaduni. Ni mchezo



Soka lenye mguso wa vurugu

Endelea uk 4

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

BURIANI RAMADHANI ATHUMANI SHAMTE (AKILI SI MALI)

Kwa masikitiko makubwa, tumepata habari za kutawafu kwa ndugu yetu, mpenzi mkubwa wa Jumuiyya ya Ahmadiyya, shujaa ambaye hakuwa na woga akitumwa kuitumikia Ahmadiyya, mshairi aliyeitumia kalamu kuwaamsha waliolala na kuwaambia ya kwamba Masihi Aliyeahidiwa amekwishafika. Mtaalamu aliyetumia kipaji chake cha uchapaji kuchapa mambo ya kheri na manufaa. Bwana aliyejikusanyia sifa zote hizi ni Bw. Ramadhani Athumani Shamte (Akili Si Mali) ambaye tulitengana nae kimwili tarehe 04/03/2018 na kuzikwa kwenye makaburi yetu Wailes Temeke na umati wa waombolezaji. Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake tutarejea.

Bw. Ramadhani Athumani Shamte alikuwa na mapenzi ya dhati na Jumuiyya ya Ahmadiyya, leta utani na masikhara lakini sio katika mambo yanahusu Jamaat, mtakosana mpaka ujirekebishe. Mapenzi yake yalimpelekea hadi kutafuta gazeti lolote au kitabu kilichoigusa Jamaat kwa ubaya, huko atakinunua kwa pesa yake na atakileta Msikitini na kumuomba Sheikh ampe dawa Mwandishi wa upotoshaji huo. Lakini alipoweza yeye hakusubiri. Hakuchelewa, alishika kalamu na kutoa jibu lililotuacha sote tumetulia na kuridhika. Sifa hii alikuwa nayo Bw. Shamte. Sifa hii inatakiwa sasa zaidi kuliko wakati uliopita. Magazeti yamekuwa lukuki, vitabu vingi vimetungwa, mitandao ndio usiseme, panahitajika Wanajamaat wanaopita hukuna huko wakitafuta mtu yeyote anayeigusa Jamaat na hapo hapo anaoneshwa njia iliyonyooka.

Bw. Ramadhani Athumani Shamte alikuwa Mshairi. Alipendwa na kuheshimiwa na wengi. Hakukosa kwenye mikutano ya Washairi na huko kwenye redio ya taifa alikwenda mara kwa mara. Lakini katika harakati zake za ushairi yeye alitanguliza Jamaat Ahmadiyya. Alihubiri Ahmadiyya. Alifafanua mafundisho ya Islam kama yanavyofafanuliwa na Ahmadiyya. Kwake sanaa hii ya ushairi ilikuwa ni silaha ya mahubiri. Silaha muhimu ya kufikisha ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as). Kuna somo kubwa kwa sisi tuliyobaki kujitahidi kutumia vipaji tulivyopewa na Allah kufikisha ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa (as). Sote Allah Ametupatia vipaji mbalimbali. Tujiulize! Ni kwa kiasi gani kipaji nilichopewa mimi kinatumika katika kupeleka mbele ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa? Swali hili alilijibu kwa vitendo Bw. Ramadhani Athumani Shamte. Nasi tukumbuke kufanya hivyo. Ada ya mja kunena, muungwana ni vitendo.

Kabla ya maradhi Bw. Ramadhani Athumani Shamte kama unavyomuona samaki baharini basi naye bahari yake ilikuwa Masjid Salaam. Hakukosa asilani. Akitoka nyumbani kwake Mwananyamala Moscow kwenye baiskeli yake kituo chake cha kwanza ni Masjid Salaam. Ataweka baiskeli yake na amuulize Sheikh kama kulikuwa na kazi yoyote apewe. Na akipewa ataifanya kwa bidii. Akitoka kazini atapita tena Masjid Salaam na kuhudhuria darasa lililokuwa linaendeshwa na Maulana Sheikh Muhammad Munawwar Chaudhry. Shughuli zote hizo zikiisha ndipo anaanza kufikiria kurudi nyumbani. Na pengine mazungumzo yangemkamata hadi saa tatu usiku. Mahali alipokuwa Hemedi Feruzi Mahmood Mbayana, Mlandura, Kibindu, ilikuwa ni vigumu kutoka. Kwa ujumla Shamte alikuwa samaki na Masjid Salaam bahari yake. Tunao wajibu nasi wa kugeuza Masjid Salaam tena sasa Masjid Salaam mpya iwe bahari ili tupate shabaha ya kuumbwa kwetu ambako ni kumwabudu Allah.

Tunaungana na Al-Ustadhi Hamisi Abdallah Mbanga (Kungwi) katika kuomboleza;

Kwetu alikuwa pete, pambo lenye unadhifu
Twamuombea apate, pepo ya Mola Raufu
Baraka zimuambate, apewe hadhi tukufu.

Al Ustadh Khamis Wamwera Akumbuka

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema Mwingi wa Ukarimu.

Jina langu ni Khamisi Sulaiman Shamte Koingato Nnyeme Wamwera. Nimezaliwa *yaumulkhamisi* ya tarehe 13 Aprili, 1938 katika kijiji cha Nyipara tarafa ya Rusende wilayani Rufiji. Masomo yangu ya shule nilianza mwaka 1950 hadi mwaka 1957 nilipohitimisha kwa kupata elimu ya darasa la nane. Nimejiunga katika Jumuiya Ahmadiyya mnamo mwaka 1955 mara tu Sheikh Swaleh Mbaruku Kapilima alipowasili kijijini kwetu. Nilikuwa mmoja miongoni mwa vijana wachache waliokuwa wameathirika na maelezo yaliyotolewa juu ya mas'ala mbalimbali ya Islam. Baba yangu mzazi hakuwa mwepesi wa kukubali ukweli wa kuendelea kwa Utume, kifo cha Seyyidna Issa a.s na ufikaji wa Seyyidna Ahmad a.s katika zama hizi. Bali baba mdogo baada ya muda alifanya Baiati na kujiunga katika Ahmadiyya. Kisha baada ya miaka kadhaa kupita, baba mzazi nae akajiunga katika Jamati.

Mwaka 1956 mjini Dar-es-salaam ulijengwa na ukafunguliwa msikiti ambao hadi sasa tunao tunaendelea kuutumia. Pamoja na msikiti huu, pia palifunguliwa chuo cha wabashiri kilicho julikana kwa jina la *Ahmadiyya Muslim Missionary College* kikiongozwa na Sheikh Kaluta Amri Abedi. Mimi nilijiunga na chuo hiki mwaka 1958 nikiwa na ndugu yangu Mwalimu Omari Abdallah Matimbwa kutoka Rufiji. Tulikuwa vijana 15 kutoka sehem mbalimbali ya Tanganyika kwa wakati huo. Sisi tulikuwa kundi la pili baada ya kundi la kwanza la akina Mzee Mwana Shemte Nyengo na Juma Abdallah Mpitakunza kumaliza muda wao. Zilikuwa siku za vuguvugu kubwa la Siasa. Ni wakati wa harakati za kudai uhuru wa Tanganyika. Waislamu pia tulitakiwa kuwamo katika msafara huu. Maulana Sheikh Mubarak Ahmad akiwa mbashiri mkuu wa Afrika Mashariki aliwahamasisha Waislam na akawahimiza Waahmadiyya wananchi kutobaki nyuma kwenye uwanja wa mchezo wa siasa. Alimwombea ruhusa Sheikh Amri Abedi kwa Khalifa mtukufu wa pili wa Seyyidna Ahmad a.s ili aingie kwenya kilinge cha siasa. Khalifa Mtukufu alikubali ombi hilo na Sheikh Amri Abedi akaingia katika siasa. Alibaki kuwa mtu wa dini pia mwana siasa. Naam alikuwa mtu wa kutegemewa mno kwenye kilio cha kudai uhuru akishirikiana na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na wengineo.

Pamoja na hayo, bado tuliendelea kuchota elimu ya dini chini ya uongozi wa Sheikh Amri hadi mwaka 1960 alipochaguliwa kuwa Meya wa kwanza Mwafrika kushika wadhifa huo katika Jiji la Dar-es-salam. Mabadiliko ya uongozi wa Jamati pia yalipatikana. Aliletwa Maulana Sheikh Muhammad Munawwar kutoka Nairobi Kenya kushika nafasi ya Sheikh Amri ambaye sasa alikwisha ingia katika uwanja wa siasa. Naam, masomo yetu yaliishia mwaka 1962 Mimi, niliteuliwa kwa kazi za Ofisini nikimsaidia Sheikh Munawar. Wenzangu walitawanywa katika sehemu mbalimbali ya Nchi yetu tayari kwa ubashiri.

Sasa tunae Sheikh Maulana Munawar H.A. Binafsi nimefanya nae kazi takriban miaka kumi hivi. Nilimfahamu vyema kwa umbile hakuwa mwembamba, bali hakuwa mrefu wa kuchusha. Alikuwa Mpakistani kwa Taifa, bali alijazwa na Khulka na mafundisho ya Kiislamu. Alikuwa mkakamavu akitazama mbele aendako. Alipenda kutembea kwa miguu. Alikuwa mvaaji wa mapajama, mateitei na yale mashati marefu. Kichwa kilikuwa kikipambwa na kilemba cheupe.

Maulana Sheikh Muhammad Munawar ni mchapakazi makini sana. Alikuwa anapenda mno kusoma vitabu na Magezeti mbalimbali; Yawe ya dini au ya dunia. Alikuwa mzungumzaji fasaha wa Kiswahili, nam sikuona vibaya kujifunza lugha hii kutoka kwake. Kauli yake ilikuwa haina tenge. Ndivyo alivyokuwa anastaajabisha watu alipokuwa anasema Kijaluo lugha mojawapo ya makabila makubwa ya Kenya. Maulana Sheikh Muhammad Munawwar H.A aliteuliwa kuwa Mbashiri Mkuu mara tu nchi hizi tatu zilipopata uhuru kwa miaka tofauti. Sheikh Munawar alikuwa Mbashiri Mkuu wa Tanganyika. Uzito wa kazi kwake uliongezeka mara dufu. Alikuwa muhodari wa kazi. Alikuwa mvumilivu mwenye maneno laini na wakati mwingine alitoa maneno ya utani. Mara zote Sheikh alikuwa mwenye wajihi wa furaha na bashasha, lakini alikuwa anabadilika hasa anapoona au kukutana na maneno ya kukashifu dini tukufu ya Islam au maelezo ya kuvunja heshima ya mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. Alikuwa mkali kwelikweli alipokuwa akiona maandiko ya kumdhalilisha Seyyidna Ahmad a.s sura yake hubadilika na lile bashasha hutoweka. Hatulii asilan mpaka atoe jibu la tuhuma hizo zilizorundikwa juu ya Islamu na viongozi wake. Wallahi nakuambia alikuwa haondoki mezani hadi anahakikisha majibu yamepatikana. Kazi hii alikuwa anaifanya hadi usiku wa manane ambapo aliacha Ofisi na kwenda kwenye swala ya Tahajjud. Asubuhi majibu ya wapinzani yalikuwa yameshapatikana kwa vipeperushi. Mara nyingi mtihani huu mimi nilianguka. Mimi nilikuwa naye hadi wakati fulani tu, baadae nilikwenda kulala nikamwacha Ofisini akiendelea na kazi peke yeke.

Katika Ibada, Sheikh Muhammad Munawwar alikuwa mfano mwema. Mara nyingi alikuwa anafunga swaumu za nafali na alikuwa anatoa sadaka za namna namna. Wakati wa swala alikuwa anaheshimu sana ule wakati ambao tulikuwa tunakubaliana ukifika, basi swala ilikuwa inasimama. Na swala ya Tahajjud ilikuwa kwake kama ya faradhi katika mwezi mtukufu wa Ramadhani ndio kabisa alikua anaongeza nguvu ya ibada zake. Naye alikuwa anatuhimiza sana kumuabudu Mwenyezi Mungu na kumtegemea. Alikuwa anatuhimiza tumuombe Mwenyezi Mungu ili watu wa nchi hii waikubali dini ya Islam na bendera yake ipepee kote duniani. Ukweli wa Seyyidna Ahmad ufahamike na wengi wao wajiunge katika Ahmadiyya. Wakati fulani nakumbuka Sheikh Muhammad Munawwar alituambia kwamba utafika wakati watu wengi watajiunga katika Jamati. Khofu na wasiwasi iliyokuwa imetanda kuwa ukijiunga katika Ahmadiyya utazikwa na nani itaisha. Sheikh alitudokeza tusiwe na wasiwasi hali ya Jumuiyya itakuwa nzuri , mambo yatabadilika "Leo" kwa wakati huo alisema Sheikh Munawwar "msikiti huu, Masjjid Salaam haujazi wanajumuiyya hata msitari mmoja tunapo swali, lakini juweni wakati utafika msikiti huu utajazwa na utaonekana kuwa mdogo maneno haya alitamka Sheikh Munawwar miaka 35 iliyopita. Wakati maneno haya yalipotamkwa yalionekana ya vichekesho. Lakini sasa maneno hayo yananihakikishia kinywani mwa Mtu wa Mungu. Hapana shaka alikuwa mchamungu na mtawa.

Sikujaliwa kuandika kila hatua. Lakini nimalizie tu kwa kusema kwamba Sheikh Muhammad Munawwar alikuwa mtu wa huruma. Vijana kadhaa walisomeshwa naye kwa kutoa karo za shule hadi kufikia Sekondari na wengine vyuo vikuu.

Alikuwa mume wa wake wawili ambao walikuwa wanafika hapa kwa zamu. Bali nyumbani mwake hapakuwapo na makubwa. Chakula chake kikubwa sana kilikuwa ni chapati na mboga ya dengu. Walikuwapo wengine wengi wakumsaidia kazi wakati wakeze hawapo naye, aliishia kwa kushukuru kwa kusema "Jazakumullah'' na shughuli kuendelea kufanya mwenyewe.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Sheikh Abdulrahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Bashart Ur Rehman
Msambazaji: Mwl. Omar Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Dr. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Kujitahidi katika Wema, Khulka Njema na Mwenendo Mzuri

Kutoka uk. 1

hatuna haki wala faida yoyote ya kujiita kuwa Waahmadiyya.

Tunapochunguza Maisha ya Mtume s.a.w. tunashuhudia viwango bora na vya kutushangaza sisi. Yeye hakupenda kabisa kwamba mke wake mmoja amfanyie mzaha mwingine juu ya ufupi au urefu wake ili asijisikie vibaya. Mara anaonekana kuwafundisha watoto khulka bora kwamba msirushe mawe kwenye miti yenye matunda na kuyapoteza matunda yasiyo iva na kuwaambia kama mnajisikia njaa kali basi mnaweza kula tende zilizoanguka chini. Pamoja na haya yote alisema kwamba ni vyema zaidi kama hamtapata hali ya namna hii ya kulazimishwa na njaa.

Kisha alimuongoza mtoto aliyekuwa anakula haraka haraka na kuzungusha mkono wake kwenye sahani yote na alimwabia soma Bismillaahi na kula kwa mkono wa kulia na kilicho mbele yako.

Tuwalee watoto wetu kwa namna hii kwamba uwongo ni dhambi na kusema kweli ni wema. Na tuwadumishe juu ya hilo toka utoto wao. Sahaba mmoja anasimulia kwamba safari moja Mtume s.a.w. alikuja nyumbani kwetu nami kutokana na utoto wangu nilijaribu kutoka nje kwa ajili ya kucheza basi mama yangu alisema kwa ajili ya kunizuia kutoka nje, njoo hapa nitakupa kitu fulani, hapo Mtume s.a.w. alimuuliza mama yangu unataka kumpa nini? Mama alijibu nitampa tende. Mtume s.a.w. alisema usingekuwa na nia hii ungekuwa mwenye kutenda dhambi ya uongo. Khalifa mtukufu a.t.b.a alisema na mtoto pia alifundishwa umuhimu wa kusema ukweli, kwa kiasi hiki kwamba aliyakumbuka hadi alipokuwa mkubwa.

Safari moja Mtume s.a.w., alimwambia mtu fulani kwamba kama huwezi kuacha maovu yote basi acha kusema uwongo. Je Waislam wa leo wameshikamana na viwango hivi vya khulka? Sisi Waahmadiyya pia tunapaswa kujichunguza, Je tumepata viwango hivi vya khulka?

Safari moja Mtume s.a.w. alieleza kwamba dhambi kubwa zaidi ni kusema uwongo na kutoa ushuhuda wa uwongo. Na aliendelea kurudia maneno haya mara kadhaa hadi maswahaba zake walitamani laiti angenyamaza.

Kisha tunashuhudia khulka zake za kuvumilia na kusubiri kwamba bedui mmoja aliaanza kukojoa katika eneo la msikiti, watu wakamkimbilia kumzuia. Mtume s.a.w. alisema muacheni na pale alipokojoa mwagieni maji, kwani ninyi ni watu ambao mmeumbwa kwa ajili ya kuwarahisishia watu na sio kuwapatia taabu. Baada ya hapo yule bedui alikuwa anamsifu sana Mtume s.a.w. juu ya huruma yake hii. Lakini siku hizi, viongozi wa nchi za Kiislam na maulamaa wao wanaendelea kuwataabisha watu.

Safari moja Mtume s.a.w. alieleza kuwa kama mnataka kujua kwamba, Je mnaendelea vizuri au vibaya, muwaulize majirani zenu kwamba wao wana rai gani juu yenu. Kisha aliwaongoza viongozi na kusema tabia zenu bora zitajulikana pale ambapo mtajihesabu kuwa watumishi wa watu. Je viwango hivi vya tabia vinaonekana katika viongozi wa leo? Viongozi wa Jamaat pia wanapaswa kujichunguza. Wakati wa ushindi wa Makka Mtume s.a.w. aliwasamehe maadui wengi japokuwa alikuwa na uwezo wa kuwaadhibu lakini wengi wao walisilimu baadae kwa kushuhudia khulka hizi za Mtume s.a.w.

Khalifa Mtukufu a.t.b.a. alimnukuu Masihi Aliyeahidiwa a.s. akieleza khulka bora za Mtume s.a.w., kwamba Mwenyezi Mungu Mwenyewe Alimwambia Mtume wetu kwamba ***Innaka la álaa Khuluqin ádhiim*** - wewe una khulka bora kabisa. Sambamba na usemi huu namna zote za khulka, ukarimu, ushujaa, uadilifu, rehema, ihsani, ukweli na uvumilivu na kadhalika, zinapatikana kwake.

Kwa kifupi nguvu zote zinazopatikana ndani ya moyo wa binadamu kama vile adabu, haya, uaminifu, ghera, uimara, utukufu, huruma, subira, kusamehe, kutoa na kadhalika, kama zinadhihirishwa sawa na wakati wake zinaitwa khulka. Tabia hizi zote ni hali za asili za binadamu ambazo zinaitwa khulka pale ambapo zinatumika mahala pake.

Sayyidna Ahmad as anasema, khulka bora zinadhihirika katika hali za namna mbili, wakati wa shida na jaribio. Sifa ya kusubiri inadhihirika chini ya radhi ya Mwenyezi Mungu na katika hali ya neema na ufalme kama anafanya uadilifu kwa unyenyekevu anaonesha khulka bora. Na hali ya namna hizi zote mbili zilipatikana kwa Mtume wetu mtukufu s.a.w. na aliweza kuonesha khulka za namna zote mbili katika maisha yake ya Makkah na Madinah. Alionesha khulka za subira na uvumilivu katika Makkah, kisha alipopata ushindi na maadui walipoletwa mbele yake aliwasamehe mara moja, ilhali alikuwa na uwezo wa kuwaadhibu.

Sayyidna Ahmad as anasema, baadhi yetu wanafanya ukarimu lakini wanawakaripia watu kwa mambo madogomadogo au kuwaelezea kwamba tumekupatia kitu. Wapo wengine ambao ni wapole lakini ni wabahili, wapo wengine ambao wana sifa ya unyenyekevu lakini sio mashujaa. Lakini mfano uliokamilika wa khulka ni mfano wa Mtume s.a.w. Ndiyo maana Mungu Alisema "**Innaka la álaa Khuluqin ádhiim**". Hivyo vipimo vya juu vya khulka vinatakiwa vipatikane kwa kila Muislam muda wowote.

Sayyidna Ahmad as anasema kama nyinyi mnaweza kuboresha khulka zenu kwa kufuata mfano huu wa Mtume s.a.w. katika mahala pake, basi ninyi pia mnaweza kuonesha muujiza. Na hakuna anayeweza kunyoosha kidole juu ya khulka bora. Ndiyo sababu Mtume s.a.w. alipewa muujiza mkubwa na wenye nguvu wa khulka zake, na mfano wake wa khulka haupatikani katika historia ya dunia nzima wala hautapatikana. Yeyote ambaye anaziacha tabia mbaya na kufuata khulka nzuri anaonesha muujiza. Kwa mfano; Mtu mkali anaacha ukali wake na kushika upole na unyenyekevu, basi anaonesha muujiza. Wapo watu wengi walioikubali dini ya kweli kwa kushuhudia miujiza ya khulka bora. Ieleweke kwamba watu wa dunia pia wanaonesha khulka kidhahiri lakini jambo ambalo linaitwa khulka kwao ni kujionesha.

Sayyidna Ahmad as alisema khulka zipo za namna mbili, namna ya kwanza ni zile ambazo zinaoneshwa na wasomi wa siku hizi, wanaoonesha upole kwa midomo yao lakini mioyo yao inakuwa imejaa husuda, khulka hizi ni kinyume cha Quran. Namna ya pili ni khulka za kweli, ambazo hazina unafiki na udanganyifu ndani yake bali zinafanywa kwa huruma ya kweli. Hivyo tuongeze viwango vya kweli ndani ya mioyo yetu.

Baadhi ya watu wanauliza juu ya wema unaofanyika kidhahiri, kama kusali sala 5 na kuonesha khulka za kawaida tu. Sayyidna Ahmad as anasema akiwajibu, khulka bora ni funguo za wema mwingine. Na tabia nzuri ni mama wa wema. Yeyote ambaye hajali khulka bora hawezi kuwafaidisha wengine. Mtu anawafaa wengine pale tu ambapo atakuwa na tabia nzuri.

Katika maisha ya kila siku, baadhi ya watu wamezoea kwamba wakimuona muombaji wanamchukia na hawatafakari kwamba kama yeye anaomba pasipo udhuru basi anatenda dhambi. Wewe kama unacho chochote basi mpe, hakuna dhambi katika kutoa. Imesimuliwa katika hadithi ya Mtume s.a.w. kwamba usimkatalie muombaji hata kama amekuja akiwa amepanda farasi, khulka nzuri ni katika kutokumkaripia muombaji. Chunguzeni kwamba wema mmoja unakuwa sababu ya kufungua mlango wa wema mwingine.

Khalifa Mtukufu alisema tunaulizwa katika jamii yetu kwamba tuwatendee vipi wazazi wetu ambao si Waahmadiyya, Sayyidna Ahmad as alisema muwaombee dua na muwafanyie wema wa kila namna, muwadhihirishie na kuwaonesha tabia nzuri mara elfu zaidi kuliko awali. Miujiza ya kikhulka inashinda miujiza mingine yote. Tuwatii vizuri katika mambo yote ya dunia na kuwahudumia kwa moyo wote na uzima wote. Kama binadamu hana khulka nzuri basi hakuna tofauti inayopatikana baina yake yeye na mnyama. Wapo watu ambao tamaa yao haiishi, wanakula mali za watu kwa njia isiyo ya halali, hawaoni tofauti baina ya halali na haramu, kama mnyama hawezi kutofautisha baina ya shamba lake na shamba la jirani yake. Hawaoni aibu katika kula mali ya mayatima, hao ndio kao lao ni Jahannam.

Kisha kuna ubaya wa kiburi unaomaliza wema wote. Kuna namna nyingi za khulka mbaya ambazo zinafutika kwa binadamu lakini kiburi huwa kinafutika mwishoni. Wapo wengi wanaoonekana wanyenyekevu lakini wanakuwa na kiburi. Baadhi wanakuwa na kiburi cha mali, wengine wana kiburi cha ukoo na wengine kiburi cha elimu. Sayyidna Ahmad as alisema kuacha khulka bora ndiyo dhambi na ndiyo dhambi inayopunguza uwezo wa kufanya wema.

Mwenye kufanya zinaa haelewi kwamba mume wa mke huyu atajisikia vibaya namna gani kwa kitendo hiki, angejua asingetenda dhambi hii, mwizi anapoiba anamaliza vifaa vyote na muda mwingine anapoteza juhudi za masikini alizozifanya kwa miezi kadhaa, angejisikia maumivu yake asingeiba.

Sayyidna Ahmad as anasema, yeyote ambaye anamwonyesha jirani yake khulka bora anaonyesha miujiza. Kisha alieleza mfano wa mtoto mzuri anayeonesha wema wa baba yake na alisema mwenye kufanya baiat anakuwa mtoto wangu. Je yeyote anapenda kwamba mtoto wake amfedheheshe baba yake? Anywe pombe na kufanya maovu yanayochafua jina la baba yake? Na kama yeyote anafanya hivyo, basi hawezi kufunga midomo ya watu. Hali kadhalika, yeyote ambaye, hajali utukufu wa silsila hii baada ya kujiunga basi ataulizwa mbele ya Allah. Hivyo basi muombe msaada wa Mwenyezi Mungu sawa na uwezo wenu wote na kufuta upungufu wenu. Na popote mtakaposhindwa basi muinue mikono yenu kwa uaminifu kwa sababu Mwenyezi Mungu hairudishi ikiwa mitupu ile mikono iliyonyooshwa kwa uaminifu. Haya tunayasema kwa uzoefu wetu. Maelfu ya maombi yetu yalipokelewa na yanaendelea kupokelewa hadi leo.

Kisha alisema bila kufanya jitihada na maombi hatuwezi kufuta giza la moyo na hakuna anayeweza kupata mabadiliko bila kujibadilisha mwenyewe kama Mwenyezi Mungu anavyosema: Inna Llaaha laa yughayyiru maa biqawmin hattaa yughayyiruu maa bi anfusihim. …. Hakika Mwenyezi Mungu Habadili yaliyoko kwa watu mpaka wabadili yaliyomo nafsini mwao.

Hivyo wanajumuiya wetu wanaweza kujibadilisha tabia zao watakapofanya jitihada na kuomba dua. Khalifa Mtukufu alisema Mwenyezi Mungu Atuwezeshe kufuata kanuni hii kwa kila namna kwa ajili ya kubadilisha hali zetu kuwa bora zaidi siku hadi siku na ubora wa khulka zote ziwe kwa ajili ya Allah sw si kwa kuwaonesha watu wa dunia. Huruma ya kweli izalike ndani mwetu kwa ajili ya viumbe vyake. Vipimo vya uchamungu viongezeke. Tuwe na fikra hizi daima dawamu kwamba tusifanye kitendo chochote kinachoweza kuchafua jina la Islam, jina la Mtume s.a.w. na jina la Masihi wake. Bali tuwe wenye kueneza mafundisho bora ya Islam na kuwavuta watu wa dunia hii kwayo. Na tuendelee kuongeza viwango vya khulka zetu kwa kuomba msaada wa Mwenyezi Mungu Aamin.

Mwishoni Huzur alisema nitasalisha sala ya Jeneza ya bwana Abdul Majiid wa Karachi Pakistan aliyefariki tarehe 15 mwezi wa Pili 2018 akiwa na umri wa miaka 88. Alikuwa mjukuu wa sahaba wa Seyyidna Ahmad as. Alisoma katika chuo cha Taalimul Islam na alijisomea elimu ya juu huko Uingereza. Kisha alifanya kazi mbalimbali za ujira na kufukuzwa kazi kwa ajili ya Uahmadiyya, basi aliamua kufanya biashara yake na kumuahidi Allah sw kwamba manufaa yote atatoa kwa ajili ya Jamaat ila kidogo tu itakayokuwa muhimu kwa ajili ya maisha. Mwenyezi Mungu Alitia baraka nyingi kwenye biashara yake lakini yeye alitimiza vizuri ahadi yake katika maisha yake yote na kutoa hela nyingi kwa ajili ya Jamaat katika mipango mingi sana. Khalifa mtukufu alimwombea dua kwamba Mwenyezi Mungu Amfunike kwa Rehma Yake na kulinyanyua daraja lake na kuwezesha watoto wake kwa ajili ya kufuata nyayo zake. Amin.

JE WAJUA? Soka Lilianzaje?

wenyenguvu ya kushawishi, kuunganisha, kufarakanisha na hata kutenganisha watu wenye dini, Taifa, kabila, hata, familia moja. Upenzi ushabiki na unazi wa soka, umekuwa ni ulevi wa aina yake ambayo huwatia kichaa wahusika wake. Kombe la dunia, linalo tarajiwa mwezi Juni nchini Urusi, ndilo tukio kubwa kuliko matukio yote ya soka duniani. Katika msimu wa Kombe la Dunia macho, masikio, na mawazo ya wengi duniani ukifuatiliwa na watu wasiopungua 30 bilioni na ukichezwa na watu wasiopungua milioni 240 kila siku.

SOKA KWA MUJIBU WA WAINGEREZA

Kuna hadhari nyingi zinazokinzana kuhusiana



Kabumbu siku za mwanzoni

na asili ya mchezo wa soka. Waingereza hushajihisha dhana hii ya kwamba Uingereza ndio nyumbani kwa mchezo wa soka (Home of the footboll game). Mwaka 1966 Waingereza walipoandaa kombe la dunia kauli mbiu yao ilikuwa *Football has come back home*- soka limerudi nyumbani. Ni ukweli ulio wazi kwamba Waingereza ndio walio uweka mpira wa miguu katika katika sura yake ya sasa. Sheria na kanuni mbalimbali za soka ziliaza kutumika Uingereza tangu karne ya 19. Imesemekana kwamba ni mnamo mwaka 1863 ndipo chama cha mwanzo kabisa duniani cha kusimamia na kuendeleza mchezo wa soka, soka kiitwacho Football Association (F.A) ndicho pia kilichosimamia mechi ya kwanza rasmi ya soka la kisasa (Modern Football) kukiwa na wachezaji 11 kila upande na kuchezwa kwa dakika 90. Mechi hii ilipigwa mnamo mwaka 1866 kati ya London na Shefield. Wanahistoria wa Kiingereza wanayo nadharia ya kuwa huenda mchezo wa soka nchini humo ulianza mnamo karne ya 2 au ya 3 ya Ukristo. Ingawa mpira wa miguu wa zama hizo haukuwa ukitawaliwa na kanuni,sheria wala mipaka ya uwanja na idadi ya wachezaji. Kwa ajili hii wana historia hao wamelibatiza soka la zama hizo kwa jina la *Mob Football*. Bila shaka ni mchezo ulioambatana na vurugu na ugomvi mkubwa! Kijiji kizima kiliingia barabarani kugombea mpira mmoja. Wachezaji walipambana mabarabarani katika maeneo ya wazi, mashambani hata katika nyua za watu. Inadaiwa kuwa mbinu yoyote iliyomuwezesha mtu kupata mpira iliruhusiwa kutumika isipokuwa mauaji tu. Hakukuwa na goli, bali kila aliyeupata aliendelea kuumiliki hadi aliponyan`ganywa. Wakati mwingine mpira ulichezwa kutoka kijiji kimoja hadi kingine na ulichezwa machweo hadi mawio. Kwa muhtasari mchezo wa soka enzi hizo ulikuwa ni kama mchezo wa vichaa. Bila shaka ni historia hii ndiyo iliyosababisha hata yule mwandishi maarufu kutoka visiwa vya West Indies auenzi mchezo huo kwa kusema:

Waingereza wanasisitiza kuwa mchezo huu ni waasili ya kizungu (Anglo saxon) na asili yake inahusishwa na miji miwili ya Uingereza, Miji hiyo ni Kingstone uliopo kando ya mto Thames na Chester. Kuna simulizi zinazoonyesha kuwa mchezo huu kwa mara ya kwanza ulichezwa kwa kukipiga mateke kichwa kilichoharibiwa cha mwanamfalme wa Kideni (Denmack) baada ya kuuawa kwake katika vita. Pia kuna nadharia inayodokezwa kwamba mpira wa miguu ulichezwa kwa mara ya kwanza katika Mji wa Derby mnamo karne ya tatu ya Ukristo katika sherehe za ushindi wa Waingereza dhidi ya Warumi. Vyazo vingine vya historia vinaeleza kuwa hata kabla ya ushindi huo dhidi ya warumi, mchezo wa soka ulishaingizwa Uingereza ukitoka katika mji wa Celtic (Scotland). Kuna nadharia zinazo onyesha kuwa hapo kabla, mchezo huu ulikuwa ukitumiwa katika mila za kipagani. Ulikuwa ukitumika kama sherehe ya kuonyesha nguvu na vipaji, wakati mwingine ulitumika kama ibada maalum ya kuombea mavuno. Kwa mpira ulifananishwa kwa taswira ya jua,nyota waliokuwa wakiabudu kama Mungu wao. Kwa hivi waligombea mpira na aliemudu kuumiliki sana kwa hiyo kwake ilikuwa kama ishara ya kujaaliwa mazao mengi. Wapagani hao walicheza mpira kuzunguka mashamba yao ikiwa ni maombi ya kulinda Mashamba hayo dhidi ya ukame na mashambulizi ya wanyama au maadui zao.

SOKA KWA MUJIBU WA FIFA

Kwa mujibu wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Duniani (FIFA) ni kwamba mpira wa miguu ni mchezo ambao umekuwepo duniani kwa miaka elfu kadhaa. Kuna ushahidi wa kisayansi unao thibitisha kuwa mchezo wa soka ulianza kama sehemu ya mazoezi ya kijeshi huko China yapata karne tatu kabla ya Ukristo. Wakati huo Uchina ulikuwa chini ya dola ya Han (Han Dynasty). Muasisi wa mazoezi hayo aliitwa Tsu Chu. Yalikuwa ni mazoezi ya kuupiga mpira kulenga uwazi mdogo uliotengenezwa kwa wavu ambao ulipachikwa juu ya mwanzi Mrefu, Mpira huo ulitengenezwa kwa ngozi na kujazwamanyoya yaliyo shindiliwa vizuri. Katika mazoezi hayo, mpigaji wa mpira alitakiwa kutumia miguu, kichwa, kifua, Mgongo na hata mabega kuupiga kuelekea katika lengo. Hii ilikuwa ni mbinu ya kuzuia mishale ya adui vitani. Matumizi ya mikono hayakuruhusiwa. Mikono



Ngozi iliyojaa hewa

ilihesabiwa kuwa ni kwa ajili ya kubebea silaha.

Aina nyingine ya mchezo wa aina hii iliyo anzia Mashariki ya mbali ni Kamari, soka la kijapani lililo anza miaka 600 baada ya ule wa mazoezi ya *Tsu Chu*. Inadaiwa kuwa mchezo huu wa kamari, unaendelewa kuchezwa hata sasa katika jadi za kijapani. Ni soka la aina yake ambapo wachezaji hujipanga Mduara wakiachana kwa umbali mfupi, kisha kupasiana mpira kwa sharti ya kuwa mpira huo usiguse ardhi. Ni kama aina fulani ya danadana ya kupasiana. Katika nchi za ulaya aina ya kwanza ya soka inaweza kuwa ni ile iliyoanzia Ugiriki, maarufu kama *Episkyros*. Hii ni aina ya soka ambayo baadaye iliingia Rumi na kurekebishwa kidogo na kupatikana aina ya soka iliyoitwa, *Harpatsum*. Ni kandanda iliyochezwa na timu mbili. Katika uwanja ilikuwa ni watu wa timu moja kuendelea kupasiana wakimiliki mpira hadi katika mstari wa mwisho wa nusu ya wapinzani wao. Ni mchezo uliohusisha nguvu, mbio na hata chenga. Ukipendwa mno zama hizo na ulidumu na umaarufu wake kwa muda wa karne 7. Baadhi ya wanahistoria wanarai kuwa mchezo huo wa *Harpatsum* ambao kwa namna fulani ulifanana na mchezo wa Raga (Rugby) ndio uliopelekwa Uingereza, ukafanyiwa marekebisho kadha kabla ya kuwa mchezo unaopendwa zaidi chini ya jua.

Pia huwa inadaiwa kuwa katika lile soka la kale (Mob Football) matumizi ya mikono kwa jinsi fulani yaliruhusiwa. Ni baada ya Waingereza kuufanyia matengenezo na kuwekea sheria, kanuni,vipimo, na muda na ndipo likageuka lulu duniani. Kwa ujumla soka sio mchezo haramu iwapo hautahusisha ushirikina, Kamari, Ugomvi na chuki baina ya watu. Kwani michezo huleta Afya na furaha, mambo ambayo Waislamu tumehimizwa kuyaendeleza.

SHURA YA KITAIFA 2018

Amir Sahib - Jamaat Ahmadiyya Tanzania, anapenda kuwakumbusha Masheikh wa Mikoa, Marais wa Mikoa, Marais wa matawi, Walimu wa Jamaat nchini na Wanajumuiya wote kwa ujumla kwamba sawa na kalenda ya matukio ya Jumuiya ya mwaka 2017/18, Majlis Shura ya Kitaifa itafanyika kwenye eneo la Jumuiya Kitonga - Dar es Salaam, siku za Jumamosi na Jumapili tarehe 28 na 29 Aprili 2018.

Matawi yote yanatakiwa yafanye vikao vya kupendekeza ajenda za Shura pamoja na kuchagua wajumbe wa kuyawakilisha matawi yao kwenye Shura hiyo ya Kitaifa. Tawi lililo na wachangiaji zaidi ya 50, linaruhusiwa kuchagua mjumbe wa ziada kwa kila wachangiaji 50 wanaoongezeka.

Marais wote wa mikoa wanahimizwa kushiriki kwenye Shura hiyo kwa gharama zao wenyewe.

Pamoja na mjumbe wa Shura atakayechaguliwa kutoka kila tawi, rais wa tawi naye pia anatakiwa ashiriki kwenye Shura ya mwaka huu.

Wajumbe wote wanatakiwa wawe wamefika kwenye eneo la Jumuiya Kitonga Dar es Salaam jioni ya siku ya Ijumaa tarehe 27 April 2018.

Ahmad ni Nani?

Na Ismail Abdul Nasibu

Mtume s.a.w alisema kwamba:
Mimi ni Muhammad, na Mimi ni Ahmad, na Mimi ni Mahi - yaan kufuru itaangamizwa nami, na Mimi ni Hashir - yaan watu watakusanywa miguuni pangu mimi, na Mimi ni Aqib ambaye hakuna Nabii baada yangu'' {Bukhari}
Hadithi hii na zingine zenye majina kadha wa kadha ya Mtume s.a.w zinaonyesha waziwazi kwamba hapo Mtume s.a.w alieleza sifa zake siyo majina yake aliyopewa alipozaliwa.
Jina moja tu alipewa alipozaliwa nalo ni jina tukufu la "Muhammad"; Lakini hadithi inaeleza majina mengi, Basi hizo zote kwa hakika ni sifa za Mtume s.a.w
Kwa kwel hakuna maana ya kuwaambia watu jina lake ilihali walilijua mapema zaid. Basi bila shaka hizi ni sifa alizotaja Mtume s.a.w zinazopatikana ndani yake.
Na kwa hiyo hata Muhammad pia katika hizo hadithi limetumika kama ni sifa ingawa hilo lilikuwa ni jina lake pia.

Basi Mtume s.a.w anaeleza kwamba yeye ni Muhammad (mwenye kusifiwa sana), na pia ni Ahmad (mwenye kumsifu sana mungu), na mahi (mwenye kuangamiza kufuru), na hashir (watu wote watakusanywa miguuni pake), na Aqiq (yaan uule ambaye hakuna baada yake Nabii mwenye Sheria).
Waahmadiyya hawajakataa siku yoyote sifa ya Mtume s.a.w kuwa mwenye kumsifu sana Mungu (yaani Ahmad); jambo tunalolikataa ni kwamba ni kwamba Ahmad sio jina hasa la dhati la Mtume s.a.w alilopewa Wakati alipozaliwa.
Tunalosema ni kwamba katika sura 61:6 Ahmad aliyetajwa ni mtu ambaye hilo jina lake, siyo tu sifa yake kwa sababu zifuatazo.-:
1) Aya hiyo hapo juu ikichunguzwa vizuri itaonyesha kwamba inawataja Manabii watatu, kwanza Nabii Isa mwenyewe asemaye, "Mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu":,
Pili yule Nabii ambaye ametajwa katika usemi huu, "Nisadikishaye yaliyomo katika Taurat" kumhusu Mtume s.a.w katika yaliyomo katika Taurat na sehemu nyinginezo za Biblia na Mtume wa tatu ni Mtume Ahmad.
Kama ukifikilia kwamba yule aliyetajwa katika Taurat (Muhammad s.a.w) ndiye Ahmad, hapo Habari ya pili ya kati utafuta- jambo ambalo huliwez kwani limetajwa wazi wazi katika aya.
Basi kwa vyovyote utalazimika kuamini kwamba Manabii watatu wametajwa. Na kwa hivyo Muhammad s.a.w ambaye bishara ya ujaji wake inasadikishwa na Nabii Isa ni tofaut na yule ambaye amebashiriwa na Nabii Isa a.s kwa kutajwa Ahmad.
2) Sababu ya pili ni kusema kwamba Ahmad katika aya hiyo siye Mtume s.a.w ni kwamba kumhusu Ahmad huyo aya inaeleza kwamba yeye ataitwa kwenye Islam;
"Na ni nani mdhalimu mkubwa kuliko yule anayemzulia Mwenyezi Mungu uwongo na hali anaitwa kwenye Uislamu". (61:8)
Aya hii inaonyesha kwamba katika zama za ujaji wa Ahmad watakuwepo watu wenye kudai kwamba wanafuata Islam. Na kwa hiyo watamwonelea Ahmad kwamba amekufuru basi watamwita aingie katika Uislamu.
Je katika zama za Mtume s.a.w walikuwepo watu waliodai kwamba



Ismail Abdul Nasibu

dini yao ni Islam? Sivyo , Basi kama mtu akisema kwamba katika aya hiyo ni sifa ya Mtume s.a.w ya kuwa Ahmad iliyotajwa, hata hivyo Habari hii haitakuwa sawa, kwani alama inayompambanua Ahmad kwamba atakaribishwa kuingia katika Islam haipatikani katika Mtume mtukufu s.a.w Bali katika Seyidna Ahmad a.s ambaye alikufurishwa na akakaribishwa kukubali ule Uislamu wao na asilimu.
Kisha aya baadaye inasema: "Wanataka kuzima nuru ya Mwenyezi Mungu kwa vinywa vyao, na Mwenyezi Mungu Atakamilisha nuru yake ijapokuwa makafir wakihirike " (61:9)
Hii yaonyesha kwamba hasa hasa maadui wa Ahmad watajaribu kumpinga kwa njia ya midomo, yaani kujibizana naye kuliko kuchukua upanga na kujaribu kumwangamiza jinsi walivyofanya wakati wa Mtume s.a.w kwamba maadui wakapigana vita vya upanga na na mishale ili kumwangamiza Mtume s.a.w ingawa maadui wa zama hizo walitumia midomo pia.
Lakini zaid sana walitia bidii kumwangamiza kwa upanga, lakini maadui wa Seyidna Ahmad a.s ingawa walijaribu kumwua kwa upanga lakini si sana, bali walijibidiisha kweli kweli kumwangamiza kwa njia ya vinywa vyao.

BISHARA YA ISA

Ni kweli kwamba Mtume s.a.w alisema kuwa Nabii Isa a.s alitoa habari njema za ujaji wake ; ndiyo ile bishara iliyoelezwa katika Injili ya Yohana 14:30:
"Mimi sitasema nanyi maneno mengi tena, kwa maana yuaja mkuu wa ulimwengu huu";
Kadhalika Nabii Isa a.s alitoa bishara ya ujaji wa Mtume s.a.w katika Mathayo 1:22-23, Mathayo 23:29, Yohana 14:16, Yohana 15:26, na Yohana 16:7-14
Nawwab Sidiq Hassan Khan wa Bhopal ameandika katika tafsir yake ya ***Fat-hul-Bayan*** j. 9 chini ya bishara ya "ismuhuu Ahmad" : katika Injili ya Barnabas habari hii imetolewa kwa maneno haya: "fedheha hii yangu na kuchekwa kwangu vitabaki hata atokee Muhammad Mtume wa Mungu".
Maneno hayo yaliandikwa kabla ya mgogoro huu kutokea kati ya Waahmadiyya na wengine, hivyo yanaweza kuamua vizuri kwamba ijapokuwa Nabii Isa a.s alitoa habari ya ujaji wa Mtume s.a.w lakini akatoa jina Muhammad.

SIFA YA KUWA AHMAD

Tuzingatie habari hii kwamba Seyidna Ahmad a.s amedai sawa na maana ya Khatamun-Nabiyiin ni kwamba yeye ni kivuli cha Mtume s.a.w kwa hivyo ijapokuwa jina hasa alilopewa Seyidna Ahmad a.s na wazazi wake ni AHMAD, Lakini vile vile mbali na jina hili Ahmad amepata sifa ya kuwa mtjme s.a.w ambayo ni Ahmad.
Yaan kwa kuacha jina alilopewa na wazazi, Seyidna Ahmad a.s kisifa pia ni Ahmad, yaani mwenye kusifu (mwenye kumsifu sana Mtume s.a.w), Jinsi ambavyo Mtume s.a.w alikuwa na sifa ya kuwa Muhammad (mwenye kusifiwa) pamoja na neno hilo kuwa jina lake pia alilopewa na wazazi wake.
Basi kila bishara au kila jambo linalomhusu Seyidna Ahmad a.s pia linamhusu Mtume s.a.w kwa hivyo, hii bishara iliyomo aya ya 7 sura 61 pia inamhusu Muhammad s.a.w kisifa, katika maana hii tuliyoeleza juu.
Yaani haiwezekani kivuli kipate sifa ambayo haimo ndani ya kitu ambacho hicho ni kivuli chake. Katika hii maana Seyidna Ahmad a.s ameandika mara kadhaa ya kwamba bishara ya 'ismuhuu Ahmad ' inamhusu Mtume Muhammad s.a.w kwani sifa zote za Seyidna Ahmad a.s zinatokana na sifa za Mtume s.a.w
Kwa hivyo hata jina la Jumuiya ya Ahmadiyya linatokana na sifa ya Mtume s.a.w ya kuwa mwenye kusifu (Ahmad); kwan katika mambo ya dini sifa ndizo zinazothaminiwa kuliko majina matupu.
Na Seyidna Ahmad a.s aliposema kuwa Jumuiya hii imepewa jina Ahmadiyya kwa sababu Mtume wetu s.a.w alikuwa na majina mawili Muhammad na Ahmad, hapo pia alikuwa ametaja sifa zake mbili za kusifiwa na kusifu.
Yaani ingawaje Muhammad lilikuwa jina la Mtume s.a.w lakini ilikuwa ni sifa yake kama tulivyoeleza nyuma. Na zama zilizopita zilikuwa za kudhihirisha Umuhammad (jalali) wa Mtume s.a.w yaan maadui walichukua silaha kuiangamiza Islam. Basi nao wakajibiwa na silaha.
Lakini katika zama hizi maadui wanataka kuangamiza Islam si kwa njia ya silaha dhahiri bali kwa njia ya elimu, hivyo zama hzi ni za kudhihiri jamali ya Mtume s.a.w; yaani zama hzi ni za kudhihirika sifa ya Mtume s.a.w kuwa Ahmad a.s
Na ili kutimiliza kazi hii Mungu Akaleta Masihi akapewa Nina hasa la Ahmad ambayo ilikuwa sifa mojawapo ya Mtume s.a.w.

MUHTASARI

Kwa ufupi ieleweke wazi kwamba Seyidna Ahmad a.s kila aliposema ya kwamba bishara ya *'ismuhuu Ahmad'* inamhusu Mtume s.a.w alikuwa na maana hiyo hiyo iliyoelezwa hapo juu. Waila pia kwamba bishara hiyo inamhusu yeye mwenyewe Seyidna Ahmad a.s (Izala -e- Auham).

• **GHULAM AHMAD**

Jina hasa la Seyidna Ahmad a.s lilikuwa ni Ahmad. Neno Ghulam ni jina la familia yake. Lakini anaposema kwamba Mwenyezi Mungu Alimwumba aliye bora kuliko Masihi Isa bin Mariam, ambaye ndiye Ghulam (mtumishi) wa Ahmad , hapo alimaanisha kuwa yu mtumishi wa Mtume s.a.w na hasa amepewa sifa ya Ahmad akiwa kivuli cha sifa hiyo iliyokuwa ya Mtume s.a.w yaani muradi wake sio kwamba yu mtumishi wa jina Ahmad bali sifa Ahmad; yaani amejaaliwa sifa Ahmad kwa sababu ya kuwa mtumishi na mtumwa wa Mtume s.a.w

• **JINA AHMAD**

Wazazi wa Seyidna Ahmad a.s walimpa jina Ahmad , na dalili yake ni kwamba baba yake mzazi alianzisha kijiji kwa jina la Seyidna Ahmad na akakiita Ahmad Abad (kijiji cha Ahmad).
Pili Seyidna Ahmad a.s kila alipochukua baiat mtu yeyote alikuwa akitamkisha
"Leo natubu dhambi zangu kwa mkono wa Ahmad";
Hakusema 'kwa mkono wa Ghulam Ahmad '
Tatu, Mara nyingi alipofunuliwa wahyi , akaitwa na Mwenyezi Mungu kwa jina la Ahmad.
Nne, akaongeza neno Ahmad pamoja na jina la kila mtoto wake wa kiume kwa mfano Fazl Ahmad , Mahmud Ahmad, Bashir Ahmad, Sharif Ahmad.
Ghulam lilikuwa jina la familia ya wazee wake kwa mfano baba yake aliitwa Ghulama Murtaza , baba zake wadogo alikuwa Ghulam Haidar na Ghulam Muhiyidin.
Basi na yeye naye akaongezewa "Ghulam" kabla ya jina lake Ahmad.
Kwa ujumla ni kwamba bishara ya sura 61 inamtaja Seyidna Ahmad a.s moja kwa moja; na pia inamhusu Mtume s.a.w kwa sababu Seyidna Ahmad a.s alitimiza bishara ya ujaji wa Mara ya pili wa Mtume s.a.w uliotabiriwa katika Kurani Tukufu (62:4), kwa hivyo Ahmad ni jina la Mtume s.a.w kwa ujaji wake mara ya pili.

Mwenye masikio na asikie!

MAKALA ZINAHITAJIKA

Bodi ya Uhariri ya Gazeti letu tulipendalo "Mapenzi ya Mungu" inawaomba ndugu wote kwamba wajitahidi kuleta makala kwa ajili ya kulipamba Gazeti letu.

Ieleweke kwamba Gazeti letu ni la kuelimisha kwa mada mbalimbali. Hivyo kwa kadri mada zinapokuwa nyingi na za kuvutia ndipo litakapokuwa na mvuto zaidi. Pia ni muhimu taarifa mbalimbali zinazotokea Mikoani ziletwe. Kwa wale wote wanaopenda picha zao zitokee kwenye gazeti watuletee nakala ya picha zao.

Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Bustani ya Washairi

NDOA

Ndoa kwa jina la bwana, naisawiri tungoni.
Ndoa jambo la maana, alonalo amewini.
Ndoa huleta sakina, na kuondoa huzuni.
Ewe Mola tuauni, tudumu na ndoa zetu.

Ndoa ni Jambo la suna, alisema Shaabani.
Ndoa kamwe si ndoana, idungayo maungoni.
Ndoa ni penzi mwanana, lizamalo mtimani.
Ewe Mola tuauni, Tudumu na ndoa zetu.

Ndoa ni kubembezana, Mtu na wake mwandani.
Ndoa si kupapurana, kama watu wa motoni.
Ndoa hujpendeza sana, watu wakishika dini.
Ewe Mola tuauni, tudumu na ndoa zetu.

Ndoa ipate kufana, pawepo na ihisani.
Ndoa si kuleteana, ya kero na hamkani.
Ndoa si kubwatizana, kwa matusi hadharani.
Ewe mola tuauni, tudumu na ndoazetu.

Ndoa si kutawalana, kwa ubabe majumbani.
Ndoa si kutandikana, makonde ya maungoni.
Ndoa kunasihiana, kwe heshima faraghani.
Ewe Mola tuauni, tudumu na ndoa zetu.

Ndoa si kukomoana, muone zaidi nani.
Ndoa sio kutegana, mtaingia fitinani.
Ndoa kuvumiliana, daima hamchokani.
Ewe Mola tuauni, tudumu na ndoa zetu.

Ndoa si kusumbuana, kwa kudai vya thamani.
Ndoa kusitahiana, hasa penye hali duni.
Ndoa ya kusimangana, huwa ni umajununi.
Ewe Mola tuauni, tudumu na ndoa zetu.

Ndoa si kudanganyana, kwa ahadi za hewanui.
Ndoa ni kuambiana, ya ukweli na yakini.
Ndoa ya wanao patina, Hubalikiwa mbinguni.
Ewe Mola tuauni tudumu na ndoa zetu.

Ndoa kukalipiana, hutoa mapenzini.
Ndoa kulaumiana, hakuleti afueni.
Ndoa ni kushikamana, muwapo matatizonil.
Ewe Mola tuauni, tudumu na ndoa zetu.

Ndoa si kufikishana, polisi mahakamani.
Ndoa si kulumbana, kwenye kesi vikaoni.
Ndoa yenye kusutana, Haidumu hasilani.
Ewe Mola tuauni, tudumu na ndoa zetu.

Ndoa kuafikiana, kwa matendo na maoni.
Ndoa sio kukwazana, na kuenzi ubishani.
Ndoa hasa kupatana, sio kuwa wapinzani.
Ewe mola tuauni, tudumu na ndoa zetu.

Ndoa ya kuchunguzana, si fundisho la kidini.
Ndoa kuaminiana, ndo nguzo yake makini.
Ndoa yenye kuwindana, huvia yake thamani.
Ewe Mola tuauni, tudumu na ndoa zetu.

Ndoa ni kufundishana, yale yanayi uauni.
Ndoa si kuingizana, kwenye uasi dhambini.
Ndoa ni kuokoana, mtoke upotevuni.
Ewe Mola tuauni, tudumu na ndoa zetu.

Ndoa mkichukiana, na mwenzio wa ubani.
Ndoa hiyo huwa laana, na kukosa Amani.
Ndoa mnapopendana, huwa pepo duniani.
Ewe Mola tuauni, tudumu na ndoa zetu.

Ndoa kuamlishana, ayapendayo manani.
Ndoa ni kukatazana, maovu ya sheitwani.
Ndoa ni kupandishana, daraja za kimbinguni.
Ewe mola tuauni, tudumu na ndoa zetu.

Ndoa mnapogomba, suluhu itafuteni.
Ndoa msije achana, huchukia Rahmani.
Ndoa mking`ang`ana, mmekamilisha dini.
Ewe Mola tuauni, tudumu na ndoa zetu.

Ndoa kungwi nimenena, nimefunda hadharani.
Ndoa wanaoikana, si wenzetu kiimani.
Ndoa tuombe sana, kwetu ziwe burudani.
Ewe Mola tuauni, tudumu na ndoa zetu.

Abdullah Khamisi Mbanga (Kungwi)

TUMTAKIE SHUFAA

1 Khabari imfikie, kila alo ndugu yetu.
Na mbaki asikie, ajue msiba wetu.
Shante Mnyeketie, amefariki baratu.
Tumuombee Shamte, ahifadhiwe peponi.

2 Shante Mnyeketie, Mwana wa biladi yetu.
Tukishughulika nae, shughuli za dini yetu.
Sambamba kienda nae, kwenye jamati yetu.
Tumuombee Shamte, ahifadhiwe peponi.

3 Amefariki ambae, Mwepesi wa kazizetu.
Wengi awahubirie, kuja kwa Masihi wetu.
Hakika kwa juhudie, sufufu wajile kwetu.
Tumuombee Shamte, ahifadhiwe peponi.

4 Kwenye ndia ya Rabuie, kutoa alithubutu.
Mitango ajitolee, ya swadaka na zakatu.
Hakuifumba yadie, kamwe hakuwa kukutu.
Tumuombee Shamte, ahifadhiwe peponi.

5 Kila tema ni swifae, swifa ndema si kurutu.
Shamte nikuambie, ali mtu hasanatu.
Mpole kwa twabiae, si mkali wa magutu.
Tumuombee Shamte, ahifadhiwe peponi.

6 Alikuwa mfanoe, wa ibada na swalatu.
Si wa tuki utukie , ali mteshi kwa watu.
Muungwana utambue, aliuthamini utu.
Tumuombee Shamte, ahifadhiwe peponi.

7 Ali mwema mpitie, Ofisi au baitu.
Si bakhili anyimae, ni mtoaji wa vitu.
Walonufaika nae, ni wengi katika watu.
Tumuombee Shamte, ahifadhiwe peponi.

8 kibindu ndoo tulie, tumlilie mwenzetu.
Yule tuloanzanae, katika pilika zetu.
Hivi sasa hatunae, maskini ndugu yetu.
Tumuombee Shamte, ahifadhiwe peponi.

9 Wamamba hebu tujie, tujae mu majalatu.
Pamoja tumuombee, tumuombee mwana kwetu.
Swahiba sura ing`ae, na aingizwe janatu.
Tumuombee Shamte, ahifadhiwe peponi.

10 Kungwi Mbanga usitae, ufike hili ni letu.
Waitwa usikawie, na wala usisukutu.
Uje duwa tumuombee, Mke si mali manitu.
Tumuombee Shamte, ahifadhiwe peponi.

11 Manoro usiatie, tumuombe mola wetu.
Shamte asiingie,naarun hamiyatu.
Tulobaki tusalie, mustaqima swiratu.
Tumuombee Shamte, ahifadhiwe peponi.

12 Shekhe tuhitimishie, Shekhe Ame nawaitu.
Nuwiya na kina sie, tuwe katika swafatu.
Shamte tumuombee, kwake pepo iwe kuntu.
Tumuombee Shamte, ahifadhiwe peponi.

13 Ya Allah utufutie, katika madhambi yetu.
Bali utughofirie, pamwe al-akhi wetu.
Amina niitikie, Amina e Mola wetu.
Tumuombee Shamte, ahifadhiwe peponi.

Al-ustadhi Mhenga Khamisi s.s. Wamwera
Kimbangulile – Mbagala Rangi tatu.

TUMEPOTEZA TURUFU

1 Innalillahi nigute, moyoni nimedhoofu.
Ametutoka Shamte, ngali mwenye insafu.
Kungwi ninapiga kite, kwa kifo cha msharafu.
Tumepoteza turufu, Bwana akili si mali.

2 Akili si mali mwite, ni lakabu maarufu.
Asili yake Utete, kwa wajuzi wa sarafu.
Wa Pwani na Bara yote, kazi zake walishufu.
Tumepoteza turufu, Bwana Akili si mali.

3 Ni mshairi kidete, mwenye beti nyofu nyofu.
Aliye wazidi kete, magwiji wa hino safu.
Akawafanya wafyate, kwenye wake ubunifu.
Tumepoteza turufu, Bwana Akili si mali.

4 Nyekefya hakuwa bwete, kwenye vita takatifu.
Penye vuta nikuvute, hakurambishwa sakafu.
Hata penye haki tete, hakuingiwa na hofu.
Tumepoteza turufu, Bwana Akili si mali.

5 Hakutaka alepwete, mbele ya waleta bifu.
Alimbana yeyote, alofanya upujufu.
Kawaadabisha wote, kwa hoja zake kunjufu.
Tumepoteza turufu, Bwana Akili si mali.

6 Hakuwa chuma ulete, yule mtu mngojefu.
Angoje wana walete, riziki ya kumkifu.
Ni kwa kapite kapite, alisaka yake mofu.
Tumepoteza turufu, Bwana Akili si mali.

7 Baba mzee Shamte, kafa na uaminifu.
Hakudhulumu mkate, wala chembe ya mnofu.
Alitafuta upate, vyake kwa uadilifu.
Tumepoteza turufu, Bwana Akili si mali.

8 Kwetu alikuwa pete, pambo lenye unadhifu.
Twamuombea apate, Pepo ya Mola Raufu.
Baraka zimuambate, apewe hadhi tukufu.
Tumepoteza turufu, Bwana Akili si mali.

9 Tangu habari nipate, kwamba kapatwa na ufu.
Nilighumiwa kitete, nikapagawa kwa hofu.
Kuwaza vipi tufute, pengo lake kwenye safu.
Tumepoteza turufu, Bwana Akili si mali.

10 Manyakanya niwaite, jitokezeni ukufu.
Tuje muenzi Shamte, ingawa kwa takilifu.
Midomo tusiifyate, bado hatujatawafu.
Tumepoteza turufu, Bwana Akili si mali.

11 Wa mamba sijikunyate, na Wamwera usikifu.
Shekhe Ame weka mate, kama wino ni pungufu.
Jipangeni tuchakate, kudumisha usanifu.
Tumepoteza turufu, Bwana Akili si mali.

12 Hapa Mbanga nijivute, japo nina udhaifu.
Maombelezo nikate, nianguke kwa Latifu.
Niombe anikokote, anijengee wasifu.
Tumepoteza turufu, Bwana Akili si mali.

Al Ustadh, Abdallah K. Mbanga (Kungwi)
Tambani – Mkulanga, Pwani.

MSIBA

Hae Msiba Mzito
Mwili unawaka moto
Ni Kaditama Ghulamu
Maarufu kwa Nujumu.

Yugenda Mzungupule
Mahiri wa Mizingile
Sisi sote wa Jalia
Na Kwake tutarejea.

Ramadhani Athumani
Katutoka duniani
Ni mapenzi ya Rabuka
Rabi Aso mshirika.

Karejea Kwake Mungu
Narome apate fungu
Twamuombea nafasi
Peponi penye nemsi.

Tamati nahitimisha
Kifo mwanzo wa maisha
Bwana Akili Si Mali
Apate yalo Jamali.

Mahmood Hamsin Mubiru (Wa Mamba)

Kuepusha Migogoro na kujenga Mahaba katika Ndoa

Kutoka uk. 1

kutumia lugha laini zenye maelewano, huku tukizingatia kuwa ni lazima mmoja wa wanandoa hao ajishushe ili kuleta masikilizano, lakini pia tusiwe ni wenye kukaa na hasira vifuani mwetu. Uzoefu unatuonyesha pia, haya mambo madogo madogo yatokeapo sehemu yoyote ile na yasiporekebishwa basi hupelekea hata kufikia kufarakana kwa wanandoa. Maana hayafanyiwi kazi kupata ufumbuzi na badala yake yakivundikwa tu, hii sio sahihi. Hali na aina yoyote ya chokochoko inapojiri ndani ya nyumba basi ni jukumu la wanandoa husika kufanyia ufumbuzi, na iwapo jambo hilo linakuwa ni nje ya uwezo basi wahusishwe watu walio na ukaribu wa ndoa hiyo. Hivyo basi, ni muhimu sana kwa mke na mume wajijengee mazingira murua ya wao kwa wao kuwa ni watatuzi wa mambo yao ya ndani, wajitahidi kuwa na sauti ya chini kwa mambo yao, wasipaze sana na kutoa sauti za ndani mwao kusikika nje. Hakika aibu yoyote katika mji, huanza kwa mke au mume kutoweza kuheshimu mipaka ya chumba chake, mipaka ya nyumba yake na kufikia hatua ya kuezua paa lake ili majirani na jamii wajue yaliyomo ndani mwao. Tutambue kuwa mapaa haya ndio yanayotutunzia stara zetu, nasi tuzitunze stara hizo ili tudumishe upendo na mapenzi ndani ya ndoa na tusishereheshe kwa yasiyowahusu. Leo hii itokeapo mume akasikia kuwa mkewe ameenda kumshitakia kwa ndugu fulani bila idhini ya mume, hakika hapo mume hukasirika sana na hata ugomvi kuanza. Wapo wanaume ambao hudiriki mpaka kutukana na kutoa kauli zisizopendeza kuzisikia. Baadhi ya wanaume hupelekea hata kuwapiga wake zao ilimradi tu kuona kama anaweza kukomesha tabia hiyo.

Mcha Mungu mmoja ambaye hatunaye duniani hivi sasa, Maulana Maulvi Dr. Abdul Wahab Adam sahib (rh) aliyekuwa ni Amir wa muda mrefu nchini Ghana mpaka umauti wake alipata kuandika kitabu chake kiitwacho REFLECTIONS: A JOURNEY TOWARDS PEACE. Katika ukurasa wa 100 ndani ya kitabu hicho ameandika kuwa 'Let us ponder over our limitations as men and women and it will make us feel humble. We will then be liberated from pride and arrogance! ' Tafsiri isiyo rasmi ni kwamba – Hebu tutafakari juu ya mapungufu yetu kama wanaume na wanawake ili tuifikie hali ya unyenyekevu. Kisha hapo tutakombolewa dhidi ya kibri. (Uk. 100 Hiki ni kitabu toleo la pili la mwaka 2010).

Nimeanza khutba yangu hii kwa kutoa mfano huu wa alichokiandika Mcha Mungu huyu Dr Wahab Adam sahib, kwani yeye aliishi mazingira kama yetu ya bara hili na alikuwa ni mtu mweusi kama sisi. Kwa neno zima, aliishi maisha ya Kiafrika kama tunavyoishi sisi leo, Mola Amrehemu.

Ndugu wasomaji,



Ndoa ni upendo. Ndoa ni furaha. Ndoa ni faraja. Ndoa ni imani. Ndoa ni amani. Ndoa ni sehemu ya ibada. Ndoa ni mapenzi.

Tukiwa ni wanaadam ambao baadhi yetu tumejaaliwa kuwa katika ndoa na tukiishi katika ndoa yaani mke na mume, hali hii ni katika kukamilisha nusu ya dini yetu tukufu ya Islam. Ndani ya ndoa zetu hizi kama ilivyo safari ya maisha kiujumla, huwepo na hali tofauti kama misukosuko fulani inayoweza kujitokeza. Hali hizo za misukosuko hutofautiana kati ya mtu na mtu, utaifa kwa utaifa, ukabila kwa ukabila. Lakini yote huunganishwa kwa imani tu ya Islam kama ambavyo Mtume S.a.w. alivyosema ya kwamba binaadam wote ni sawa, hayupo aliye m'bora zaidi ya mwingine.

Ndoa zote huongozwa na amani na upendo uliosheheni mapenzi ya dhati kwa wanandoa, ndipo hushamirisha mji husika. Hapo mwanzo tumeaswa kwa kupitia nukuu ya Maulvi Wahab Adam sahib juu ya unyenyekevu katika ndoa ili tukombolewe kutoka katika hali ya kibri, maringo na majigambo. Mcha Mungu huyu anatuonyesha ya kwamba iwapo hali zetu za ndoa zinazongwa na mazingira ya kujiona mmoja wa mwanandoa awe mke au mume kuwa ni bora zaidi ya mwenzake, hali hiyo huwa ni chembe za kibri, jambo ambalo hatupaswi kuwa nalo ndani ya ndoa zetu kwani huanza kuzalisha hisia hasi kutoka kwa mmoja wa wanandoa. Bali tumeaswa sana juu ya unyenyekevu wa kutambua hii ni ndoa yangu, inayonihusu na ni sehemu ya Uislamu wangu, basi yatupasa sote tuweze kujawa imani mbele ya Allah, tukiikosa imani ndani ya nafsi za nyoyo zetu basi hapo tutambue kuwa tayari tutafungulia mlango wa kutetereka. Imani ndani ya ndoa huepusha misukosuko yoyote kujitokeza, kwani nyote wanandoa mtaongozwa kwa kufuata mafundisho sahihi ya Mtume Mtukufu Muhammad Mustafa S.a.w.

Mwanaume kama kiongozi wa nyumba analazimika ajitambue juu ya hilo na kisha anatakiwa afuate mambo kadhaa ya msingi ikiwemo kuipatia familia matumizi na mahitajio stahiki kiujumla. Mwanaume anapaswa awe ni mwema zaidi kwa mkewe na vizazi vyake, amjali mke wake na hali zake za mapungufu aliyonayo, awajali watoto kwa upendo wa hali ya juu kabisa. Awaonyeshe upendo na uwajibikaji kama baba, kama mume ndani ya ndoa. Yeye akiwa ni baba anatakiwa kutoa malezi mazuri kwa watoto na mke pia, ili kutoa fursa kwa wanafamilia nao wajifunze yaliyo mema kutoka kwa mume na baba yao. Hali hiyo hujenga urafiki, ukaribu na hudhihirisha mapenzi baina ya mume na mke. Huwajengea mapenzi na huruma baina ya baba na watoto, huondoa wigo wa kuogopana na kutokumkaribia baba. Kwa kupitia aina ya khulka njema za baba hupelekea kwa kila mwanafamilia kuanza kujifunza na kujua majukumu yake hususan pale watoto nao wajaaliwapo kupevuka ilhali baba akiendeleza hali ya kutekeleza majukumu ya kila siku ipasavyo. Hali zote hizo hunawirisha na kuhuisha amani, utulivu na upendo ndani ya nyumba husika na zaidi kwa wanandoa.

Kama kweli sisi wanaume tunahitaji utulivu majumbani mwetu, utulivu katika ndoa zetu, basi yatupasa tujitazame hali za tabia na khulka zetu kwanza. Iwapo tutabaini ni khulka gani tulizonazo, basi itakuwa ni njia rahisi ya kujitambua na kujirekebisha, kisha tutaanza kuona hali za mabadiliko majumbani mwetu kuelekea maelewano na furaha, lakini kwanza tujitathmini na tutathmini hali na nyendo zetu.

Katika moja ya khutba zake, Hudhuur (a.t.b.a) alisema: "Iwapo wewe ni hodari sana wa kufanya mahubiri, kuhubiria wenzako, kujituma kazini na katika utafutaji mali, lakini iwapo nyumbani kwako hauna khulka njema basi ni khasara tupu." Yatupasa sisi waume kujitathmini hali zetu, na Insha'Allah nitaelezea mwishoni mwa khutba yangu hii hali ambazo sisi waume yatupasa kuzingatia katika maisha yetu ya kawaida ya ndoa zetu, kwa uhalisia.

Baadhi ya wanaume ambao kwa kujijua kuwa wao ni viongozi majumbani mwao, huanza kubadilika na kuleta dharau kwa wake zao, jambo hili la dharau ni baya na halifai kwa mke wala kwa mume, hayupo apendae kudharauliwa. Hali hii ipo na inadhihiri kila kukicha na kupelekea misukosuko kujiri, lakini chanzo cha haya yote ni kutokufuata mafundisho sahihi ya Mtume S.a.w. ili tujifunze ni kwa namna gani Mjumbe huyu wa Allah aliweza kuishi na wake katika mazingira tofauti sawa na hali za nyakati, lakini wote aliwaonyeshea upendo, aliwathamini, aliwatunza na aliwahudumia. Tumepewa Mtume S.a.w. kuwa ni mfano bora, yatupasa sisi wanaume tujitutumue na tujifunze hali ya maisha yake yalivyokuwa. Japokuwa hatuwezi kufikia kiwango cha wema wa Mtume S.a.w. kwa wakeze, lakini walau tujitahidi kusoma maisha yake na tujirekebishe, Allah Mtukufu Atatusaidia.

Tunajifunza kuwa japo Mtume S.a.w. alikuwa na majukumu makubwa sana ya Utume, lakini hakuwa nyuma katika kuzijali familia zake na kuwajali wakeze. Dunia ya leo tunashuhudia mtu akipata kibarua kidogo tu, hugeuka na kuwa ni kama vile amepewa kibali cha kuanza kibri ndani ya nyumba yake. Akichelewa kurudi nyumbani, akitumia muda mwingi kwa marafiki kuliko kumkimbilia Allah, akibagua vyakula, akimtoa kasoro mkewe, baadhi hufikia hata kunena "naona kama vile wewe haukunistahili vile, hauendani nami vile". Siku hizi, mtu mwenye kazi ndogo tu aliyojaaliwa sawa na elimu na maarifa yake, hugeuka na kuwa kana kwamba ndie mtu aliye na wajibu mkubwa sana kimajukumu kazini kwake na kupelekea kutokuwa na muda kabisa wa hata kuisikiliza familia yake, kwamba akipigiwa simu au kutumiwa ujumbe mfupi basi mke ataelezwa yu '*busy*', ndipo hufikia hata wake zetu nao kupelekea kukimbilia apate na afanye kazi ili kuenda sawa na mume. Je, ni nani mwingine aje na atokee ili kuijali familia yako na mke wako au wake zako kama si wewe mwenyewe mume?

Nikimnukuu Hudhuur (a.t.b.a) alipata kusema katika moja ya khutba zake kuwa: "Ili mke awe ni mwema na Mchamungu au awe mwenye adabu njema, inalazimu kwanza mwanaume ndio aonyeshe hali ya Ucha Mungu na kuwa ni mtu mwenye matendo mema". Ikizingatiwa kuwa mwanaume amefanywa kuwa ni kiongozi kwa mke (kwa mujibu wa Qur'an), maadili yake yanatakiwa kuwa ni mema, awe ni mwenye imani. Hii hutoa fursa kwa mke wake pamoja na watoto wake kuanza kufuata vitendo vizuri vya mume na baba yao, na hatimae kupelekea mji na nyumba hiyo kunawiri kwa wema na bashasha. Inafaa tutambue pia kuwa, "mke hujifunza kutoka kwa mume kwa kila tendo alifanyalo, likiwa jema atafuata

Endelea uk 8

Kuepusha Migogoro na kujenga Mahaba katika Ndoa

Kutoka uk. 7

na likiwa ni baya atafuata pia". Yote haya yanahitaji muongozo mwema utokee kwa mwanaume. Wanaume tujitahidi kufanya matendo mema yenye athari, na tuwe na matendo mema. Wake zetu huzijenga nyumba zao kwa kupitia tabia zetu wanaume, tabia zetu ndio maisha ya nyumbani tunapotoka. Tujitathmini sisi wanaume na hali zetu.

Mtume S.a.w. aliwafundisha watoto wake na wake zake kuhusu Umoja wa Mwenyezi Mungu. Hakuwahi kutumia nguvu katika kuwaelekeza wake zake na hata watoto wake. Mtume S.a.w. aliwaeleza wakeze na wanafamilia yake kuwa jukumu lenu ni ibada ya Mwenyezi Mungu na kuimarisha Tauhid. Alikuwa pia akiwaamsha wakeze kwenye swalat nyakati za Fajr, hata kwa kuwanyunyizia vijimaji kidogo ili waamke na watekeleze ibada ambayo ndio lengo la kuumbwa kwao. Zipo elimu ambazo tunafundishwa pia kuwa Mtume S.a.w. alikuwa akiwasaidia wakeze kazi za nyumbani, jambo ambalo hata sisi hatuhitaji kuwa na darja la Utume ili tuweze kuwasaidia kazi za nyumbani wake zetu na kuwahurumia. Tusiwatendee dhulma wake zetu wala tusitumie makaripio ama lugha zenye kuudhi na chembe ya ukali. Bali huruma kuu itutawale na sote tujue fika juu ya hali za wake zetu na namna walivyoumbwa. Inatupasa sisi wanaume tuongoze katika kuwa na subra njema, tuwahurumie wake zetu, tuwahurumie wake zetu, tuwahurumie wake zetu. Tumuombe sana Allah Mtukufu Atujaalie subra njema pamoja na unyenyekevu, na kwamba tuishi maisha yaliyotawaliwa na unyenyekevu katika kuyaelekea mambo na hususan pale chembe za misukosuko inapodhihiri, Allah Mtukufu Azijaalie nyumba zetu zisiwe ni fukuto la moshi unaoumiza macho na kutiririsha machozi, na kukimbiza watu. Mke na mume akitawaliwa na subra, basi mambo yenye kheri nyingi yatakuwa nasi na InshaAllah hata Malaika watazitembelea nyumba zetu, bali tutaona mtiririko mkubwa wa wageni kuja kututembelea. Pia tuwahurumie viumbe wenzetu hasa pale itokeapo tukaitwa kuwa ni sehemu ya wasuluhishi katika baadhi ya migogoro ya ndoa, hekima na busara zinatuhitaji sana.

Ndugu wasomaji, Tunazidi kuona mfano kuwa, Mtume S.a.w. alikuwa akishona nguo zake mwenyewe, akishona viatu vyake mwenyewe, alikuwa akitenengeneza hata ndoo ya nyumbani mwenyewe pale inapoharibika. Haya ni mapenzi ya hali ya juu ambayo tunajifunza kutoka kwa Mtume S.a.w.. Zote hizi ni sehemu ndogo tu ya kazi za nyumbani ambazo Mbora huyu wa viumbe anatufundisha juu ya kutekeleza majukumu ya waume kwa wake zake. Lakini hii leo, sisi wanaume tumegeuka majumbani mwetu na kuwa ndio wafalme tusioweza hata kupeleka ndoo ya maji bafuni ili wewe mwenyewe uoge, hatuwezi kwenda gengeni kumsaidia mke pale anaponyonyesha au pale anapobanana kwa kufua nguo, ya kwamba hata kuchukua maji kwenye fridge pia tumekosa uwezo huo na kutugeuza kuwa ni wafalme katika ndoa zetu. Hii si sahihi, inatupasa sisi wanaume tuchunguze hali zetu na imani zetu mbele ya Allah. Na wapo ambao hatuwatendei haki wake zetu basi yapasa tujichunguze na tujue kabisa kuwa tayari tunao mtihani wa kutetereka kiimani. Namuomba Allah mtukufu atunusuru na mtihani huo.

Naomba nimnukuu tena Hudhuur (a.t.b.a) pale aliposema kwenye moja ya khutba zake kuwa: "Wanaume mnatakiwa kukubali makosa madogo madogo ambayo wake zetu wanawaeleza pale mnapokosea". Sisi wanaume ni wanaadam na hivyo hatujakamilika kama jinsi ambavyo wanawake wasivyokamilika pia. Tujitahidi sana kutafuta suluhu za haraka na tusijikweze wala kujitutumua sana mbele ya wake zetu hawa, wanahitaji huruma na tuwahurumie sana, tuwapende sana wake zetu. Wema huu ndio hushamirisha upendo ndani ya ndoa zetu na kuondoa mafundo na madukuduku vifuani mwetu. Je utajisikiaje ewe mume kuona ukitamka neno moja tu na kumuona mkeo akidondosha machozi kwa ajili yako, kwa maumivu ambayo umemsababishia, akilia kwa kwikwi. Je huu ndio mradi wa wewe kumuoa na kuja kumdondosha machozi kila mara? Je tunakumbuka vema khutba za ndoa na Aya zinazotumika wakati wa ndoa jinsi zinavyotetemesha vifua pale ndoa inapoidhinishwa na kuridhiwa na Allah Muumba wetu Mtukufu, tutafakari sana. Ndoa si mfano wa mchezo unaopita na kufutika, ndoa inanukuliwa na mbingu. Tusizichezee ndoa zetu.

Ipo hadithi moja ya Mtume S.a.w. iliyosimuliwa na Hadhrat Abu Hurairah r.a. ya kwamba Mjumbe wa Allah S.a.w. alisema: "Mkamilifu zaidi wa imani miongoni mwa waaminio ndiye aliye na khulka njema zaidi kuliko wengine." Na "mbora wenu ndiye awatendeaye vizuri wakeze." Hapa tunafundishwa tabia na maadili mema zaidi ya kuwatendea wake zetu, na kwamba haturuhusiwi hata kuwa na sehemu ya tabia za kuwafinya, kuwafokea na hata kuwapiga wake zetu, bali hali zao tuzitambue na tuepushe misukosuko ndani ya miji yetu ili kulinda imani mbele ya Allah. Pia hakuna mahala popote tulipofundishwa ya kwamba mke wako akikukwaza basi umfokee na kumtolea maneno makali, hakuna hilo. .

Imesimuliwa na Hadhrat Aas ra ya kwamba Mjumbe wa Allah S.a.w. hakutukana wala hakupenda wengine watukane. Na alikuwa anasema – Hakika wabora wenu ndio wale walio na khulka bora kati yenu (Bukhari). Tujitahidi sana.

Ndugu wasomaji, Seyidna Ahmad a.s. alisema: "Wafuasi wangu hawatakiwi wawe na tabia hii ya kuwapiga wake zao. Maana wapo wanaume ambao wanazo tabia na khulka za kupiga wake zao, na iwapo utatumia maneno makali kwa mke wako basi fanya Istighfar. Wapo wanaume ambao wanawapiga sana wake zao mpaka kuwajeruhi. Hapa Mtume S.a.w. alituasa kuwa watu wa namna hiyo basi wanatakiwa wachunguze zaidi imani zao. Ikiwa mtu imani yake haikukamilika, basi anaweza kupotea wakati wowote". Hali zozote hasi ambazo tunaweza kuzifanya dhidi ya wake zetu basi tutambue kuwa hazitujengi, bali zinachagiza misukosuko zaidi na hekaheka ndani ya nyumba. Mola Azinusuru nyumba zetu zisipotee shauri ya misukosuko.

MFANO MMOJA HAI: Ndugu Abid Khan (*Press Secretary* wa Hudhuur) alipata kusimulia kuwa, siku moja wakiwa katika safari ya kikazi na Hudhuur nchini Ujerumani alipata kuulizwa na Hudhuur kwamba "Abid, habari ya familia yako. Abid akajibu kuwa nashukuru ni salama. Mkeo hajambo? Akajibu, naam hajambo. Hudhuur akamwambia palepale kuwa hebu muandikie ujumbe wa simu na umwabie mkeo ya kwamba unam-miss. Hudhuur akamwambia muandikie maneno ya ***I MISS YOU***. Abid Khan akatekeleza kama alivyoshauriwa na Hudhuur. Alipoandika na kumtumia mkewe ujumbe ule, haraka sana mke wake aliujibu ujumbe huo, aliujibu kwa bashasha na mshangao mkubwa. Wakati akiwa anamaliza kuusoma ujumbe huo, mke wake Abid akaandika ujumbe mwingine tena kuwa, hivi ujumbe huu ulioniandikia ni kwamba umeshauriwa na Hudhuur? Yaani Hudhuur ndio amekuambia unitumie ujumbe huo? Hapo ndugu Abid Khan akabaki ameduwaa tena, ya kwamba huyu mke wangu amejuaje kama ni kweli Hudhuur ndio amenishauri nimtumie ujumbe ule? Ila mke wake alibaki na bashasha na furaha nyingi ndani mwake. Baadae Hudhuur alikuja kumuuliza Abid, ilikuwaje baada ya kumtumia ujumbe mkeo? Ndugu Abid Khan papo hapo akajibu alikuwa ni mwenye furaha sana. Hudhuur akamwambia, mimi ninajua majukumu yako Abid ni mengi na muda wako ni mfupi, pia ninajua kuwa wewe hauna khulka ya kumwandikia mkeo ujumbe mzuri na aupendao kama ule." Somo ambalo tunafundishwa sisi wanaume kwa kupitia mfano huu ni kwamba tusiwaache nyuma wake zetu hasa pale tunapotingwa na majukumu mengi, basi tutenge muda walau hata wa kumtumia ujumbe wenye kumfurahisha ili amani imtawale na nyakati zote ajue kuwa anajaliwa. Pia tunafundishwa kuwa, wake zetu hupenda kupokea jumbe nzuri zenye upendo kutoka kwa sisi waume zao.

Iwapo mwanaume anayedumu katika sala nyakati zote akiwa nyumbani kwake na akiamka kusali nyakati za usiku huku akilia kwa kuongea na Mola wake, basi matendo hayo hukaa akilini mwa mwanamke na hupelekea kumjenga na kumbadilisha mke huyo ambapo naye taratibu huanza kupata khofu ya Allah nae akaanza kusali. Mfano huu ni moja ya njia na nyendo njema ambazo yatupasa kwanza sisi wanaume tuzidumishe majumbani mwetu ili tutoe athari njema kwa wake zetu, athari ambazo zitachagizwa zaidi na upendo kwa utulivu wetu. Tukijua fika kuwa wake zetu ndio walezi wakubwa wa watoto wetu, athari hizi za tabia njema huwawia rahisi hata watoto wetu kuiga kutoka kwa mama zao ambao mara zote huwa karibu yao kuliko wawavyo karibu yetu akina baba. Kwani, wake zetu ndio wanaoshinda majumbani nyakati zote na wanetu. Hivyo hizi athari njema si tu zitamsaidia mume mwenyewe na mke, bali zitasaidia kulea watoto ili waje kuwa ni watu wema hapa duniani huku wakichukulia mifano ya maisha mema na yenye upendo waliyoyashuhudia kutoka kwa wazazi wao.

Wapo wanaume ambao majumbani mwao hudumu kuangalia vipindi vya luninga visivyopendeza, tena huviangalia vipindi hivyo kwa muda mrefu tu. Itokeapo kwa baadhi ya mwanaume akakumbushwa tu kwa wema kutoka kwa mkewe, basi hapo wanaume hubadilika na kuwa ni wakali na kutoa maneno makali kabisa. Baadhi ya sisi wanaume hufikia na kutoa maneno makali kabisa pasipo stara na kujikuta watoto wetu wameketi na wakisikiliza jinsi baba anavyofoka na kutoa maneno yasiyopendeza. Ikumbukwe, kwa mazingira hayo ya ufokaji mbele ya watoto wetu basi watoto bongo zao hunasa, hufyonza na kubakisha kumbukumbu akilini, na hali hiyo ikidumu sana basi hupelekea wanetu kuanza kumdharau baba na kutokuwepo mapenzi nae. Watoto wengine hudiriki na hata kufikia kusema kuwa 'sasa muda wa mzee mkorofi kurudi umekaribia au kusema mzee mkorofi yule anakuja na kujifungia vyumbani mwao. Yote haya husababishwa na khulka za mume kwa mkewe.

Ipo nukuu ya Mcha Mungu mmoja isemayo: mwanaume halisi humsitiri mkewe hata katika sala, na yule asiye na wivu humuacha tupu katika masoko wala hajali. Nukuu hii inazidi kutufundisha wajibu wetu waume kwa wake, kwamba tuwakumbuke katika sala zetu na kuwajali. Inawezekana kwa kuwakumbuka wake zetu katika sala zetu zinaweza kuwabadilisha hali zao na kuepusha migogoro na migongano kadhaa wa kadha. Na itokeapo hali ya migogoro au hali yoyote ile ya kupishana, basi yapasa sisi wanaume tuikumbuke hadithi hii Iliyosimuliwa na Hadhrat Abu Hurairah ra ya kwamba Mjumbe wa Allah S.a.w. alisema: Mwaminio asimchukie mkewe mwaminio. Kwani kama khulka yake moja inamchukiza basi anayo khulka nyingine ya kupendeza pia. (Muslim)

Itaendelea toleo Lijalo

Safari Hiyo!

Na Mahmood Hamsin Mubiru

Siku ya mauti kuja, mtu hana kimbilio
Kuja budi itakuja, kama si kesho ni leo
Kila mtu humfuja, pasi ya mapendeleo
Habaki mtu mmoja, katika safari hiyo.(Shaaban Robert)

Ni Jumapili ya tarehe 04 mwezi wa tatu 2018. Nje pana mvua za rasharasha. Usiku palikuwa na upepo mkali na wa kutisha. Bila shaka ukiashiria mambo kadhaa. Namaliza kusali Subuhi. Napanga vitu vyangu vizuri na kuhakikisha nimebeba kila nilichokihitaji. Nina maradhi ya kusahau. Nachukua bodaboda hadi kituo maarufu kiitwacho Chama. Naelekea Kitonga kwa kupitia Chanika. Kwenye kituo chetu Kitonga kuna semina muhimu ya malezi kuhusiana na ndoa iliyotayarishwa na Naib Amir Bw. Issa Mwakitalima Sahib. Ni semina iliyopewa matangazo ya kutosha na haikutakiwa mtu akose pasi na sababu ya msingi. Ni safari tulivu kwani magari hayajawa mengi barabarani. Kwenye milango ya saa moja tunafika Chanika. Ninashuka kuelekea kituo cha mabasi yanayokwenda Mbagara. Siku hiyo mabasi si mengi hivyo nalazimika kupanda Bajaji hadi Mvuti.

Kabla sijafika mbali simu yangu inaita, nami siisikii kwa haraka kwani ninasoma kitabu cha Khalifatul Masih II Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad (ra) "Blessings of Khilafat" (Baraka za Ukhalifa). Simu inaendelea kuita na hatimae naipokea. Sauti hainipotei hata kidogo. Ni ya Bw. Kassim Maftah ambaye tulijuana ujanani toka mwaka 1965 wakati yeye akiishi Kigamboni na mimi nikiishi Masjid Salaam. Moja ya sifa kubwa ya Bw. Maftah inyeshe mvua au jua kali lakini akijua kuna mgonjwa lazima atakwenda kumtizama. Anatoa; Assalaam Alaikum Bw. Mubiru. Waaleykumsalaam Bw. Maftah. Ndugu yangu Bw. Ramadhani Athumani Shamte katutoka. Kwa sauti ya huzuni naitikia; "*Innaalillahi wa inna ilaihi Raajiuun*". "Vipi mipango ya mazishi" Namuuliza. Ananieleza ya kwamba mipango hiyo inafanyika na suala zima kwa hivi sasa limo mikononi mwa Jamaat. Roho yangu imetulia. Naiweka simu mfukoni. Machozi yananitiririka! Na yananipeleka hadi mwaka 1965 nilipokutana kwa mara ya kwanza na Bw. Ramadhani Shamte (Akili si mali). Haikuwa vigumu hata kidogo kuzoeana na kuelewana na Akili si mali kwani daima alikuwa na bashasha na aliyependa kubadilishana mawazo. Na kwa sababu ya khulka hiyo sikuchelewa kumuuliza; kwanini alipendelea lakabu hiyo ya 'Akili si mali'. Alinieleza ya kwamba watu wanakosea sana; akili ni kitu chenye thamani kubwa kuliko mali. Ni akili inayotengeneza mali. Kwa hiyo huwezi kulinganisha akili na mali. Wakati tunajuana mimi na yeye Bw. Shamte alikuwa anafanya kazi idara ya uchapaji Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam. Nami nikiwa mwanafunzi wa kidato cha kwanza. Wanajamaat kwa siku hizo tulikuwa wachache na hivyo ilikuwa ni rahisi kujuana na kuwa na mazungumzo. Lakini la msingi zaidi ilikuwa ni vigumu kwa Bw. Shamte kukosa Msikitini. Atatoka nyumbani kwake Kinondoni Moscow kwenye baiskeli yake iliyokuwa pembeni imeandikwa 'Mke si mali, fanya kazi' na akiingia ataifunga kwenye mkungu na kuirudia jioni. Siku hizo itakumbukwa kulikuwa na tatizo kubwa la usafiri. Yeye hilo alilimaliza kwa baiskeli yake. Katika mazungumzo yake yote alionesha mapenzi makubwa na yasiyotetereka juu ya Ukhalifa. Na aliipenda sana Jamaat kwa kiwango kikubwa. Jukumu la kuchapisha habari za Ahmadiyya alilibeba yeye na jarida hilo lilikuwa linatoka kila mwisho wa mwezi na kwa wakati.

Mapenzi yake kwa Jumuiyya yalijidhihirisha katika Nyanja zifuatazo:-Ramadhani Athumani Shamte hakuwa na rafiki wa kutaja nje ya Jamaat Ahmadiyya. Marafiki zake na ndugu zake walikuwa Waahmadiyya. Furaha yake ilikuwa kuwa miongoni mwa Waahmadiyya. Wakibadilishana mawazo na kuelezana njozi mtu alizozipata, kitabu alichosoma na gazeti alilolisoma. Kimsingi ulikuwa ni urafiki wa fikra na kupanuana mawazo. Enzi hizo vitabu vinavyopotosha juu ya Jamaat Ahmadiyya vilisakwa kwa udi na uvumba na vilipopatikana vikasomwa na kutolewa majibu ya kina. Hicho ndicho kilikuwa kipindi chake Shamte. Na ukimkuta hapo furaha tele moyoni. Marafiki zake wa karibu zaidi katika Jamaat walikuwa ni pamoja na Mohammed Saidi Kibindu



Mzee Ramadhani Athumani Shamte enzi za uhai wake

ambaye aliwahi kuwa Katibu Mkuu wa Jamaat Bw. Hemed Mahmood Feruzi Mbyana ambaye alikuwa ni Mwalimu wa Jamaat na alimsaidia Sheikh Mubarak Ahmad katika kuhariri gazeti la Mapenzi ya Mungu huko Nairobi. Ukiwakuta hao huwezi kubanduka. Kiswahili ilikuwa mali yao. Wakizungumza kwa madaha na mbwembwe na la kufurahisha wote hao walikuwa Washairi tena Washairi wa kina. Waandishi wazuri wa makala, watunzi wa vitabu na watafsiri wa vitabu. Mwalimu Hemedi Mbyana ndiye aliyetafsiri "Invitation to Ahmadiyyat" (Mwito kwa Mfalme Muislam) na pia ndiye aliyeandika kitabu cha "Mwana Aliyeahidiwa" pamoja na kitabu cha ***Ndoa ya Kiislam*** na pia alikuwa ni mtunzi mzuri wa mashairi. Rafikiye mwingine wa karibu alikuwa ni Mohammed Saidi Kibindu ambaye ni mshairi mzuri na mwandishi hodari wa makala. Bw. Kibindu ametafsiri vitabu kadhaa kikiwemo ***Yesu Katika India*** cha Masihi Aliyeahidiwa (as) na kitabu cha ***Yesu Kafia Wapi*** cha Sheikh Jalaludin Shamsi. Bila shaka kama wasemavyo Waswahili ukikaa karibu na waridi utakosaje kunukia? Kwa Ramadhani Athumani Shamte ushairi haikuwa sanaa ya mchezo hata kidogo, ilikuwa ni silaha muhimu na madhubuti. Ni silaha ya amani na ni silaha ya kufikisha ujumbe kuhubiri na kuadibu jamii. Nakumbuka kila Mbashiri alipowasili nchini alikaribishwa kwa shairi lililosomwa katika tafrija ya kumkaribisha Sheikh huyo. Ilikuwa ni desturi katika siku hizo Mbashiri kukaribishwa kwa tafrija. Ambapo hotuba zilitolewa na mashairi kusomwa. Na shairi la Ramadhani Athumani Shamte halikukosa asilani. Na hata walipopata likizo ya kwenda Pakistani aliwaaga kwa mapenzi na huba. Fani hii ya ushairi pia Bw. Ramadhani Shamte aliitumia vilivyo katika kuwajibu wapinzani. Na alijitahidi sana kuwakumbusha Wanajamaat mambo ambayo yalikuwa ni ya msingi katika Jamaat yetu. Ramadhani Athumani Shamte alikuwa ni Mshairi. Alikuwa ni Mshairi mwenye dira na msimamo. Katika maisha yake yote ya ushairi alitawaliwa na Qur'an Tukufu na Sunna za Mtume Mtukufu Muhammad (s.a.w.). Kalamu yake ilielekeza katika kufikisha ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as). Al Ustadh Hamisi Sultani Wamwera alitoa kilio juu ya zama hizi, zama za hatari. Zama za vita. Zama za tufani. Zama za mafuriko, akawaita washairi nini la kufanya! Na hasa ni ni maana ya zama hizi? Mshairi mmoja akatoka na; Hizi ndizo zile zama, zilokwishatabiriwa Kwa bishara za hashima, bingwa wa kufafanua Kuwaunga maasuma, mwanzo walofunuliwa Zilikwishatabiriwa, ndiyo hizi zile zama. Nae Ramadhani Athumani Shamte alishika kalamu na kuzungumzia zama hizi;

1. Zama hizi za mashaka, waume na wanandani
Uchao kupapatika, nguo zawekwa kichwani
Kiangazi na masika, twashuhudia machoni
Zama hizi za gharika, twazisoma vitabuni.
2. Zama hizi za gharika, twazisoma vitabuni.
Dunia imechafuka, watu hatuelewani
Huruma imegeuka, vita chini na angani
Zama hizi za gharika, twazisoma vitabuni.

3. Nawaeleza kafika, Masihi wa Qur'ani
Kaja ondoa twarika, vikundi havipatani
Aomba kukubalika, tuacheni upinzani
Zama akheri zamani, zamani hizi ni zama

Alililolisisitiza zaidi Ramadhani Athumani Shamte (Akili si mali) ni kumpokea Masihi Aliyeahidiwa (as) na akawaita kwa kusema; "pandeni safina hii ya Nuhu wa zama hizi"

Mlio mkimngoja, mwasubiri kwa makini
Kama lini itakuja, iegeshe bandarini
Wamrima na unguja, na sisi tuwe chomboni
Pandeni safina hii, ya Nuhu wa zama hizi.

Safina yenyewe ni Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya. Mkishapanda Safina hiyo anaendelea kusema Ramadhani Athumani Shamte (Akili si mali), la msingi na la lazima ni kuishika kamba ya Ukhalifa. Bila Ukhalifa hakuna Islam. Hakuna maendeleo. Na kamba ya Ukhalifa ndiyo mkombozi wetu. Ramadhani Athumani Shamte (Akili si mali) anafafanua;

1. Kukiangua kicheko, ndugu zangu purikeni
Kutamba huko na huko, huwezi anguka chini
Mbele yake nyuma yako, ya kupasa kubaini
Shikilia kamba hii, hadhari isiponyoke.
2. Kamba yataka mweledi, mjuzi wa kila fani
Tena afanye juhudi, asubuhi na jioni
Asijifanye inadi, kujigamba hadharani
Shikilia kamba hii, hadhari isiponyoke.
3. Kamba hii ukishika, uishike kwa makini
Wangapi waloanguka, leo hawajulikani
Hata tukiwakumbuka, hawana yao thamani
Shikilia kamba hii, hadhari isiponyoke
4. Kamba ina utelezi, kama hujui baini
Usishike kipuuzi, sikia yangu ilani
Atujalie Mwenyezi, hadi twende kaburini
Shikilia kamba hii, hadhari isiponyoke
5. Kamba inataka mali, ya shamba na mfukoni
Kamba usiwe bakhili, utaharibu imani
Alichokupa Jalali, mpe yeye Rahmani
Shikilia kamba hii, hadhari isiponyoke

Shamte alikuwa shujaa na imara katika imani yake. Hakuna masikhara hata kidogo katika kueneza ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as). Katika hili hakuwa na woga hata chembe. Ili kuelewa hoja tunayojaribu kuijenga juu ya ushujaa wake tutizame kwa ufupi kazi nzuri iliyofanywa na Jamaat katika kutetea maslahi ya Islam katika Tanzania. Na baadae tutaona alipohusika moja kwa moja alipohusika Bw. Ramadhani Athumani Shamte (Akili si mali). Itakumbukwa ya kwamba Padre Dale wa huko Unguja alitoa tafsiri ya Qur'an Tukufu kwa Kiswahili ambayo haikuwa na chochote isipokuwa kashfa na kubeza dini tukufu ya Islam. La kushtua na kusikitisha zaidi ni kwamba baadhi ya Masheikh katika Afrika Mashariki walishangilia na kuipokea Qur'an hiyo kwa mikono miwili. Lakini mtaalamu wa Ahmadiyya Sheikh Mubarak Ahmad alipoisoma kwa haraka akaona upungufu mkubwa uliyomo katika tafsiri ya Qur'an hiyo. Na hivyo akajidhatiti kujibu shutuma zote na kuyaweka bayana mafundisho matukufu ya Dini ya Islam. Huo ulikuwa ni utetezi wa hali juu. Ahmadiyya pia iliiandikia Serikali ya Kikoloni katika miaka ya 1940 kuhusu wafungwa Waislam waliokuwa jela wakati wa mwezi wa Ramadhani. Waliomba ya kwamba Waislam wapewe kazi zilizo nyepesi katika mwezi mtukufu wa Ramadhani. Jumuiyya pia ilitoa malalamiko yake

Endelea uk. 10

Namna Bora ya Kutumia Mali

Na Musa Mgeleka.

Na umpe ndugu haki yake, na maskini na msafiri, wala usitapanye (mali yako) kwa ubadhiri.

Hakika watumiao kwa ubadhiri ni ndugu za mashetani; na Shetani ndiye asiyemshukuru Mola wake.

Na kama unatengana nao kwa kutafuta rehema ya Mola wako unayoitumai, basi sema nao kwa maneno laini.

Na wala usiufanye mkono wako ufungiwe shingoni mwako kwa ubahili uliokithiri, wala usiukunjue kwa ubadhirifu mkubwa; usije ukaishia katika hali ya kulaumiwa na kufilisika.
Surah 17:27-30

PESA Hutumika kwa ajili ya Kuendesha FAMILIA, SHUGHULI/ BIASHARA NA KUJITOLEA. Ukiacha Kukidhi haja ya Makusudio haya Huo huitwa UBAHILI na Ukitumia Kupitiliza Haja yake huo Huitwa UBADHIRIFU wa MALI. Haja za Matumizi ya Pesa zote Hutegemeana kwa pamoja. Hivyo Unaweza Ukawa Bahili kwa Kutimiza jambo moja tu na Kuacha mengine. Baadhi ya watu wengi wamejikita Kutumia Pesa Kuhudumia Familia



tu na Kuacha Kujitolea au Kuhudumia Shughuli zao. Ubahili na Ubadhirifu ni mambo mawili yanayotegemeana. Maana Ubahili Umetangulia na Kufuatiwa na Ubadhirifu. Kuwa Ukifanya Ubahili kwa Kujitolea au Kushughuli zako basi Utafanya Ubadhirifu katika Matumizi ya Familia.

Ili Ubahili Usiwepo na Ubadhirifu basi yakupasa Kugawa Kipato chako katika Mafungu Matatu ya Kuendesha Shughuli zako, Familia na Kujitolea. Na ndio maana Katika Michango ya Mikubwa ya WASIA Mwisho Kutoa ni 1/3 zaidi ya hapo Huruhusiwi Kutoa. Ikimaanisha zaidi ya 2/3 zitumike kuendeshea Familia na kazi zako. Hali hii ipo tu kila hali na ndio maana Kujitolea kupo wakati wa Faraja na Dhiki maana Usipojitolea wakati wa Dhiki Utafanya Ubahili na Ubadhirifu sehemu fulani.

Ubahili Unamadhara kwa Uchumi na kama ilivyo Ubadhirifu - Kutumia Hovyo ulivyo na Madhara.

Matumizi ya Familia yapo kila siku ila Mali haina Uhakika wa Uwepo wa kila siku. Hivyo Unapopata Mali weka sehemu kwa ajili ya shughuli zako ili Kuhakikisha Uhakika wa Mali kila siku kwenye Matumizi yako kwenye Familia.

KUJITOLEA HUJENGA BIASHARA/ SHUGHULI, URAFIKI NA UOMBEZI (2:255)

Hivyo usipojitolea Uhakika wa Kustawi shughuli yako Hupungua na Kuanguka. Hivyo Athari ya Ubahili kwenye hatua moja huangamiza hatua yenzake ambayo ni tegemezi kwa hatua nyingine. Ubahiri umeitwa Ndugu wa Shetani 17:28 ndio Huua vipawa vyote vya maendeleo kwa Kuamusha Dhana Ubadhirifu / Mtumia Hovyo Mali. Waswahili husema Pesa ni Shetani Ukiwa na Pesa zilizorundikana hazina kazi basi hukupelekea kwenye Matumizi ya Hovyo. Sio mtu, Taasisi au Serikali Bahiri iliyoweza Kufanikiwa ila zote ziliishia kwenye Maangamio kama ilivyo Uchumi wa ghari sana na wenye Matumizi makubwa mwisho wake ni anguko.

Tunamuomba Allah Aturahisishie Kutimiza Malengo ya Kutafuta Mali. Amin

ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA

"Kumbukeni ya kwamba hakuna atakayeshuka toka mbinguni.

Wapinzani wetu wote waliopo hivi sasa watakufa na hakuna mmojawapo atakayemuona Yesu mwana wa Mariam akiteremka kutoka mbinguni.

Baadaye wazao wao watakaowarithi pia watakufa bila ya hata mmoja wao atakayemwona Yesu mwana wa Mariam akishuka toka mbinguni. Kadhalika watoto wa wazao wao nao watakufa bila kumwona mwana wa Mariam akiteremka toka mbinguni.

Hapo Mwenyezi Mungu Atatia wasiwasi katika nyoyo zao, ya kwamba siku za utukufu wa msalaba tayari zimepita na dunia imeingia katika hatua mpya, ilhali mwana wa Mariam bado hajashuka toka mbinguni.

Na hapo wale wenye busara miongoni mwao wataitupilia mbali imani hii, wote kwa pamoja.

NA KUANZIA HII LEO KARNE YA TATU HAITAKUWA IMEPITA ambapo wale wamngojeao Yesu haidhuru wawe Wakristo au Waislamu, wataudhika mno na kukirihika na kuiacha imani hii mbovu. Na kutabakia na dini moja na kiongozi mmoja tu.

Mimi nimekuja kupanda mbegu. Mbegu tayari nimeipanda kwa mkono wangu. Sasa itamea na kukua na hakuna awezaye kuizuia".

Tazkiratush-shahadatain, uk. 65, Oktoba, 1903).

MANENO YA BUSARA

Ukijaaliwa kutuliza kichwa chako, wakati wote wanaokuzunguka wamekuwa hamnazo, na wanakulaumu wewe kwa hali yao hiyo. Ukiweza kujiamini wakati wengine wote hawana imani na wewe na ukavumilia na ukastahamili kwa msimamo wako huo. Au watu wakikuhadaa nawe usijiingize katika uchafu huo. Au unapochukiwa lakini ukawapenda hao wanaokuchukia. Na wala hujioneshi kwamba umefanya wema wowote na wala hujigambi kwamba wewe una busara sana. Ukiwa na njozi-fikira za mbali lakini usitawaliwe na njozi hizo. Ukiwaza kutafakari lakini usitawaliwe na fikra hizo bali ukapiga hatua ya kutekeleza fikra zako. Ukiweza kukutana na ushindi au kushindwa na usiwatofautishe maadui hawa wawili na uwaone wote sawa. Ukiweza kuvumilia ukweli uliosema unapindishwa au kuona vitu ulivyopigania maishani vinateketea lakini ukajikusanya tena na kuanza tena upya bila kusema chochote au kulalamika. Ukizungumza na umma na akina yakhe na ukazungumza na wafalme na ukiona wote kuwa ni binadamu. Kama ukishika yote niliyosema ulimwengu huu utakuwa wako na ndio njia ya kuwa MPIGANAJI

Safari Hiyo

Kutoka uk. 9

juu ya mfumo wa elimu uliyokuwepo enzi hizo za ukoloni. Mfumo huo ulikuwa ni kuzipatia ruzuku shule za Mission – shule ambazo hazikuwaruhusu watoto wasio Wakristo kujiung ana shule hizo. Jumuiyya ya Ahmadiyya ilisema hatua hiyo haikuwa nzuri kwa sababu Waislam walikuwa wanatoa kodi na kodi hiyo ndiyo ilikuwa inakwenda katika shule za Mission ambapo wao walikuwa hawaruhusiwi kujiunga na shule hizo. Jumuiyya ya Ahmadiyya pia ndiyo iliyoomba Waislam wapewe rukhsa ya kusali Ijumaa na waweze kupewa siku kuu wakati wa Eidil-Adh'ha. Hata hivyo ushujaa wa Ramadhani Athumani Shamte ulijitokeza mwaka 1971 wakati Serikali ilitoa muswada wa Sheria ya ndoa na talaka. Muswada huo ulikuwa na baadhi ya vipengele ambavyo Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya haikuridhika navyo. Hivyo palikuwa na mushawwara miongoni mwa Wanajamaat na hatimaye Sheikh Muhammad Munawwar aliandika waraka wa kuonesha upungufu katika Muswada huo sawa na mafundisho ya dini tukufu ya Islam. Katika waraka huo Sheikh Muhammad Munawwar alisisitiza ya kwamba Waislam siku zote wanaongozwa Qur'an Tukufu na suna za Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.). Ilishauriwa ya kwamba Serikali isifanye haraka kupitisha muswada huo kuwa sheria hadi watu wameusoma na kuuelewa vizuri. Pia Sheikh Muhammad Munawwar alieleza ya kwamba muswada huo uliokuwa umeandikwa katika Kiingereza ufasiriwe kwa Kiswahili ili watu watoe mawazo yao bila ya kikwazo cha lugha. Baadhi ya vipengele ambavyo Shiekh Muhammad Munawwar alivigusia ni pamoja na; Ibara ya 13 iliyoeleza ya kwamba Msichana aolewe akifikisha miaka 15, Sheikh Munawwar alipinga wazo hilo. Kwa kusema ya kwamba kinachotakiwa kusemwa hapo ni kwamba ubalehe ndiyo dalili ya kutosha ya msichana kuweza kuolewa. Na hilo ndilo jambo la busara zaidi. Pia kuna ibara iliyogusia juu ya mke na mume wakishakaa pamoja miaka 2 basi hiyo tayari imekwishakuwa ndoa. Sheikh Munawwar alisema ya kwamba huo ni ufuska. Waraka huo ulichapwa vizuri na wa kutosha na hivyo ukatakiwa upelekwe katika Bunge la Tanzania ili wapatiwe waheshimiwa Wabunge. Itakumbukwa ya kwamba katika enzi hizo Bunge lilikuwa linakutana katika ukumbi wa Karimjee ambao upo mjini Dar es salaam. Baadhi ya Wanajamaat walionesha wasiwasi wao, lakini Ramadhani Athumani Shamte bila woga wowote akiongozana na Sheikh Muhammad Munawwar walifika katika ukumbi wa Karimjee na kuanza kutawanya waraka huo. Jambo la kufurahisha mno ni kwamba Wabunge walianza kutumia hoja zilizotolewa na Waraka kutoka Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya. Jambo lililomfanya Bw. Rashidi Mfaume Kawawa kiongozi wa Serikali katika Bunge kulaani na kusema ya kwamba kuna kikundi kidogo cha Makadiani wamesambaza vipeperushi ambavyo sasa vinatumiwa na baadhi ya Wabunge. Kwa hali yoyote ile Bw. Ramadhani Athumani Shamte alifanikiwa kufikisha tena kwa ujasiri mkubwa maoni ya Islam katika Bunge la Tanzania. Ushahidi mwingine wa ujasiri wa Bw. Ramadhani Shamte ulijitokeza mke wake alipokwenda Bagamoyo. Akiwa huko mama huyo alijifungua na mtoto hakuwa riziki. Watu wa pale alipofia huyo mtoto walikataa katakata kumzika mtoto huyo kwa kigezo ya kwamba yeye ni mtoto wa Ahmadiyya. Shamte alipofika hapo na kusikia tuhuma zao hizo alichofanya ni kuomba maji akamkosha na kumvika sanda halafu akawaomba wamuoneshe mahali gani pa kuchimba kaburi na akachimba kaburi na kumzika mtoto wake. Watu walikuwa wamemzunguka wakistaajabu hayo yaliyokuwa yakitokea mbele ya macho yao. Bila ya hasira yoyote alipomaliza shughuli zote aliwatolea salam na kuondoka. Hii ni mara ya pili katika historia ya Wanajamaat nchini Tanzania kususiwa na maiti. Tukio la namna hii lilifanyika miaka ya 1970 huko Bukoba ambako Sheikh Hafidh Suleiman alifiwa na mwanae na watu wa Bukoba wakakataa kushiriki katika mazishi hayo na sheikh Hafidh Suleiman akakamilisha yote anayotakiwa kufanyiwa maiti.

Itaendelea toleo Lijalo

Mambo Muhimu ya Kuzingatiwa Katika Shura

Kutoka uk. 12

na huendelea kurejea yale yale yaliyokwishasemwa na wengine. Ni muhimu kwanza usikilize wengine wanasemaje, ulinganishe usemi wao na kisha ndipo utoe wazo lako. Hata hivyo usitegemee mawazo ya wengine. Hivyo mtu asitoe wazo kwa ajili ya mtu mwingine wala kuwa na wazo kwa msingi wa wazo la mtu mwingine. Kwa mfano kama mtu anajaribu kuonesha kasoro fulani basi usimuunge mkono tu, bali uifikirie wewe mwenyewe kasoro hiyo na kisha ndipo utoe wazo lako.

8. Mtu asiwe na uhakika kuwa mawazo yake ndiyo yanafaa na wala hayana kasoro yoyote. Baadhi ya watu hufanya kosa hilo na jambo hili huwafanya watoke kwenye ukweli. Mara nyingine hata watoto wanaweza kuwa na mawazo mazuri ya kustaajabisha. Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w) alikuwa anashauriana hata na wake zake. Baada ya makubaliano ya Hudaibiya, wakati watu walifadhaika sana na wakakataa kuchinja wanyama wao, Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w) alimuuliza Hazrat Umm-e-Salama (r.a) afanye nini? Alimshauri akachinje mnyama wake bila kusema lolote kwa yeyote. Alifanya hivyo na watu wote wakamfuata na kuchinja wanyama wao. Hivyo mtu asisisitize juu ya wazo lake, kwani hata watu wenye uzoefu wanaweza kufanya makosa na mara nyingine mtu wa kawaida akaweza kutoa wazo zuri na lenye manufaa. Mtu akae katika kikao hiki kwa shabaha ya kuongeza elimu yake. Hata hivyo si sahihi kukubali kila wazo linalotolewa na mtu. Kubali tu kile ambacho kinaingia akilini na ukatae kile ambacho hakiingii akilini.

9. Daima tunza ukweli akilini mwako. Watu wengine huamsha jazba za watu wengine ambao ambao hushindwa kuona uhalisia wa mambo. Mimi pia niliwahi kutumia jazba za watu lakini nilijenga hoja. Mkutano uliwahi kufanyika kujadili kufungwa kwa Madrasa Ahmadiyya. Wakati kila mmoja aliunga mkono rai hii, mimi nilisimama kuipinga kwa kutoa hoja zangu. Kwa mfano nilisema kama hatuna wasomi wetu wa dini tutakimbilia wapi kufutu maswali ya kidini? Niliwaeleza kwa unyenyekevu kuwa Madrasa Ahmadiyya ilikuwa imeanzishwa kwa kumbukumbu ya Masihi Aliyeahidiwa na watu watasema nini tukiifunga Madrasa hiyo katika Jalsa ya kwanza baada ya kifo chake? Nilipomaliza kila mtu alikubali ya kuwa Madrasa Ahmadiyya isifungwe. Hata Khawaja Sahib ambaye alitoa hoja hiyo ya kufungwa kwa Madrasa Ahmadiyya alisema hakuwa na maana hiyo. Hivyo kuamsha hisia ili kuunga mkono hoja inaruhusiwa, lakini ni kukosa uaminifu kutegemea hisia peke yake na kujaribu kubadili maoni ya watu. Hivyo yule anayejua kuwa hoja yake ni dhaifu na bado anaamsha hisia za watu, anafanya kosa la kutokuwa mkweli.

10. Kunaweza kuwa na mapendekezo ya aina mbili, yale yanayoleta faida kubwa ya kidini na yale yanayoleta faida ya kidunia. Kwa vile sisi ni Jamaat ya kidini, lazima tuunge mkono mapendekezo yanayoleta faida kubwa ya kidini.

11. Siku zote tuweke jambo hili maanani, kuwa mawazo yetu siyo tu yawe mazuri, bali yawe ya kiwango cha juu kuliko yale ya wapinzani wetu. Pia kazi zetu ziwe za kudumu kuliko zile za wapinzani wetu. Kwa mfano tukijenga nyumba mbali na mkondo wa mafuriko haidhuru hata kama haitokuwa imara lakini kama imejengwa karibu na mkondo wa mafuriko, nyumba hiyo lazima iwe imara. Hivyo mapendekezo yetu katika shura yasiwe tu chanya, bali yawe na nguvu ya kutosha kupambana na wapinzani wetu. Zaidi ya hayo ni muhimu kuwa mapendekezo yetu yawe bora kuliko mapendekezo yetu katika kipindi kilichopita. Mataifa huanguka yanaposahau moja ya mambo haya mawili. Kama ilivyotokea kwa Waislam wakati unaweza kuja wapinzani wetu wakawa dhaifu na ikiwa wakati huo utakuja na juhudi zetu si bora kuliko zile zilizopita, sisi pia tutapata hasara kubwa. Ulikuwepo wakati Waislam walikuwa dhaifu, lakini ulikuja wakati ambao maadui zao walikuwa dhaifu na Waislam wakawa wenye nguvu, wakati huo Waislam walikuwa na nguvu kuliko hata Wakristo, lakini licha ya nguvu zao wakadhoofika kwa sababu hawakuwa na vikosi vya kutosha. Hivyo tunatakiwa tuendelee kuongeza nguvu zetu ama sivyo tutashindwa. Kwa mfano ikiwa mpinzani amesimama na sisi tunatembea bila shaka tutampita, lakini kama mpinzani akija anakimbia nasi tunaongeza tu hatua, bila shaka atatupita. Wakati huo tutahitaji kukimbia kuliko yeye. Labda taifa lijitakie laana kutoka mbinguni ama sivyo taifa hilo haliwezi kamwe kuangamizwa ikiwa linahakikisha kuwa mipango yake siyo tu bora kuliko ya adui zake lakini pia mipango yake hiyo ni bora kuliko ile ya wakati uliopita. Hivyo ni muhimu kuzingatia mambo haya mawili.

12. Jambo la kwanza la kuangalia wakati wa kujadili pendekezo ni kuona kama lina manufaa au la. Watu hupoteza wakati mwingi kuzungumzia vitu visivyo vya msingi ambavyo havina uhusiano na pendekezo lililotolewa. Jiepusheni na hoja zisizo na uhusiano na pendekezo. Weka fikra zako zote kwenye pendekezo husika.

13. Labda unalotaka kusema liwe na uhusiano maalum na mada inayojadiliwa, la sivyo jiepushe kurudia yale ambayo tayari yamekwishasemwa. Si lazima kila mmoja azungumze isipokuwa pale ambapo ana jambo jipya la kuzungumza.

14. Chunga muda wako na muda wa wengine.

Kutoka Kitabu cha 'Taratibu za Shura ndani ya Jamaat Ahmadiyya".

Mradi Mkubwa wa Maji Wazinduliwa Jamia

Kutoka uk. 12

Morogoro, Mwakilishi wa Mamlaka ya Maji Morogoro (MOROWASA), ofisa wa kata pamoja na safu yake ya viongozi, wenyeviti wa mitaa ya kata ya Kihonda Maghorofani, waandishi kumi wa habari wa vyombo vya habari kama vile TV, radio, magazeti nk. Sheikh Basharat-ur-rahmaan sahib mkurugenzi wa Kiwanda cha uchapishaji cha Jumuiya ya Ahmadiyya, Sheikh Asif Mahmood Butt sahib Sheikh wa mkoa wa Morogoro, Dr. Fazlurrahman mkurugenzi wa hospitali ya Jumuiya – Morogoro, wanafunzi na waalimu wa shule ya Jamaat msingi na chekechea, wanafunzi na wahadhiri wa chuo cha Jamia Ahmadiyya pamoja na majirani.

Hafla ilianza majira ya saa 4:30 asubuhi kwa usomaji wa Kurani tukufu iliyosomwa na Mwareje Muhammad.

Kisha ilifuata ripoti fupi ya mradi na utambulisho wa wageni waalikwa, kazi ambayo ilifanywa na m/kiti wa sherehe hiyo Sheikh Abid Mahmood Bhatti sahib ambaye pia ni mkuu wa chuo chetu cha Jamia Ahmadiyya – Morogoro katika ripoti yake, Maulana Sheikh Abid sahib ameainisha gharama za mradi kuwa ni jumla ya Shilingi Milioni Mia Moja na Hamsini zimetumika. Aliongeza kusema kuwa, baada ya kazi ya uchimbaji wa kisima na maji kupatikana yalichukuliwa sampuli na kupelekwa katika maabara kwa ajili ya kuyapima, na AL-HAMDU-LILLAAH majibu ni mazuri na mamlakka inayohusika imetoa kibali kinachothibitisha ubora na usalama wa maji haya na kuongeza kuwa yanafaa kwa matumizi yote ya nyumbani.

Baada ya ripoti hiyo, m/kiti wa hafla alimkaribisha mkurugenzi wa taasisi ya IAAAE bwana Akram Ahmad sahib ili kuzungumza machache.



Amir sahib akimsindikiza Mkuu wa Mkoa wa Morogoro na msafara wake wakati wakipita karibu na mnara ambao umebeba tenk la Maji.

Katika maelezo yake, bwana Akram sahib amesema kuwa ni agizo la Khalifa mtukufu a.t.b.a kwa taasisi hiyo yakuwa ishughulikie na kutatua changamoto zinazo wakabili wananchi wa bara la Afrika. Hivyo amesema yeye na wafanyakazi wa taasisi ya IAAAE wanajitahidi usiku na mchana kutekeleza agizo la khalifa mtukufu katika kuwaondolea wakazi wa bara hili changamoto zinazowakabili.

Aliwaomba wasikilizaji wawaombee dua za kheri wafanyakazi wa taasisi hiyo ili watekeleze vyema majukumu yao.

Baada ya hapo m/kiti wa hafla Sheikh Abid m. Bhatti sahib alimkaribisha mgeni rasmi ili kuwahutubia wahudhuriaji, katika hotuba yake mgeni rasmi aliishukuru na kuipongeza Jamaat kwa kuonyesha moyo wa ukarimu na mapenzi katika kuwajali, kuwathamini na kuwapenda wananchi – kwa jitihada kubwa zinazofanywa na jumuiya kuwapunguzia kero ya maji wananchi. Alisema, popote uendapo hapa nchini ukiwauliza wananchi tatizo lao kubwa ni nini? Watakuambia maji, maji, maji. Aliendelea kusema kuwa pamoja na jitihada kubwa za serikali katika kutatua suala hili, bado changamoto ni kubwa, hivyo zinapojitokeza taasisi kama hii kuunga mkono serikali ni jambo jema. Alisema upatikanaji wa maji katika mji wa Mororgoro ni asilimia 71 Na lengo la serikali ni kuhakikisha inafikia asilimia 95- hivyo bado safari ni ndefu. Mheshimiwa mkuu wa mkoa aliwataka wananchi na viongozi wa serikali wanao zunguka mradi huo waweke mikakati maalum katika kusimamia na kulinda miundo mbinu ya mradi ili uwasaidie kwa muda mrefu. Alisisitiza kuwa mmesaidiwa maji bure, haitapendeza kuona kuwa hata koki ikiharabika muwaombe waliowaleteeni mradi wawatengenezee- hii ni aibu.

Pia katika hotuba yake, mheshimiwa mkuu mkoa aliipongeza sana jamaat kwa kufuata taratibu na kanuni za kuyapima maji haya na kuthibitishwa ubora na usalama wake kwa matumizi ya binadamu. Alisema kama hatua hizo zisingefanyika hangekuwa tayari kuuzindna mradi huo. Hivyo aliishukuru jumuiya kwa kuwapatia maji wananchi, lakini pia kujali afya zao kwa kuhakikisha maji haya ni salama.

Alisema ingawa hatuna cha kuilipa jumuiya hii, lakini ni vizuri viongozi wa serikali ya mtaa kuiandikia barua ya shukrani jumuiya ya Ahmadiyya kwa msaada huu muhimu. Aliwataka viongozi hao wafanye hivyo kabla hata mkurugenzi wa IAAAE hajafunga safari ya kurudi London - UK

Baada ya hotuba ya mgeni rasmi, m/kiti wa hafla alimkaribisha Ameer na mbashiri mkuu Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry sahib ili kuzungumza na wahudhuriaji , katika hotuba yake Ameer sahib aliwa shukuru waandaaji wa hafla hiyo kwa jinsi walivyojitolea kuifanikisha vyema. Na kwa namna ya pekee kabisa alimshukuru sana mheshimiwa mkuu wa mkoa kwa kukubali mwaliko wetu pamoja na kwamba alipewa muda mfupi kabla ya sherehe yenyewe yaani siku moja kabla. Pia Ameer sahib alifafanua msimamo na mlengo wa jamaat kote duniani. Alisema kwamba Jumuiya ya Ahmadiyya haijihusishi na masuala ya siasa, bali siku zote inaunga mkono na kutii serekali iliyopo madarakani. Aliongeza kusoma kuwa msimamo wetu huu umetujengea taswira nzuri nay a kuaninika katika nchi zote duniani.

Mwisho Ameer sahib aliongoza maombi ya kimya na kuhitimisha haffla hiyo ambayo ilifanya vizuri sana.

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

JUM II - RAJAB 1439 AH | MACHI/APRIL 2018 | AMN./SHAHD. 1397

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Abdullah bin Amr bin Aas r.a. ya kwamba Mjumbe wa Allah s.a.w. hakutukana wala hakupenda wengine watukane. Na alikuwa anasema: Hakika bora wenu ndio wale walio na khulka bora kati yenu (***Bukhari***)

Mradi Mkubwa wa Maji Wazinduliwa Jamia

• Wananchi Kuchota Maji Bure

• Serikali Yaipongeza Jamaat Kupunguza Kero ya Maji

Mwenyezi Mungu Anasema, "Na bila shaka wakati ujao ni bora kwako kuliko uliopita". (93:5)

Tena Mwenyezi Mungu Alimwambia Masihi Aliyeahidiwa a.s, "Upanue mahali pako".

Hakika maneno hayo ya Mwenyezi Mungu ni mwujiza mkubwa ambao unaendelea kutimia siku hadi siku na sisi ni mashuhuda wa kutimia kwake. Bila shaka huu ni uthibitisho wa ukweli wa Masihi Aliyeahidiwa as. kwani Kurani tukufu inasema, "Hakika wale wanaomtungia Mwenyezi Mungu uwongo hawafaulu". (10:70)

Hivyo basi kuendelea kupanuka na kustawi kwa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya ni dalili tosha na madhubuti kabisa juu ya ukweli wa mwanzilishi wake. Zaidi ya hayo, Hadhrat Sayyidna Ahmad as akielezea juu ya Fadhili, Neema na Baraka nyingi za Allah zilizokuwa zikimshukia kama mvua ya masika, alisema :- "Kulikuwa wakati ambapo makombo ya watu yalikuwa ndio chakula changu, lakini leo kwa fadhili za Mwenyezi Mungu ninalisha jamaa wengi,"(AINA-E-KAMALAAT ISLAM)



Mkuu wa Mkoa wa Morogoro akikata utepe katika ufunguzi wa mradi wa maji huko Jamia uliodhaminiwa na taasisi ya IAAAE. Kulia kwake ni Amir na Mbashiri Mkuu pamoja na Mwenyekiti wa Taasisi ya IAAAE barani Ulaya Mhandisi Akram.

AL-HAMDULILLAH, kwa fadhili na baraka nyingi za Mwenyezi Mungu, Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya kupitia taasisi yake ya IAAAE imejenga mradi mkubwa na wa kisasa wa kisima kirefu cha maji safi na salama ktk eneo la chuo cha Jamia – huko Kihonda ktk Manispaa ya mji wa Morogoro. Mradi huu ulianza kwa uchimbaji wa kisima chenye urefu wa mita 140 kazi ambayo ilifanyika mnamo mwezi wa Februari mwaka 2017. Na kazi za utandazaji wa mabomba, kutengeneza stand yenye urefu wafuti 35 kwenda juu kwa ajili ya kuwekea matanki 2 yenye ujazo wa lita 5000 kila moja, kufunga solar nk, zilifanyika na kukamilika mwanzoni mwa mwezi Februari mwaka 2018.

Wanufaika wa mradi huu ni wanafunzi wa chuo chetu cha Jamiah Ahmadiyya, Waalimu na Masheikh wote, wanafunzi na waalimu wa shule yetu pamoja na wakazi wanaozunguka eneo letu la Jumuiya ambao wamewekewa kituo maalumu cha kukinga maji kwa ajili yao.

KUZINDULIWA KWA MRADI

Mradi huu ulizinduliwa rasmi siku ya Jumatatu ya tarehe 26/02/2018. Mgeni rasmi katika hafla hiyo iliyofanyika katika eneo la msikiti wetu wa Kihonda, alikuwa ni mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Dr. Kebwe Steven Kebwe.

Wageni mbalimbali waalikwa na waliohudhuria katika hafla hiyo ni Sheikh Tahir M. Chaudhry, Amir na Mbashiri Mkuu nchini, Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Morogoro mjini mheshimwa Hassan Nania, Mkurugenzi wa taasisi ya IAAAE Akram Ahmad sahib kutoka UK, Mhandisi wa Maji mkoa wa Morogoro, Ofisa wa Mamlaka ya Maji mkoa wa

Endelea uk. 11

Mambo Muhimu ya Kuzingatiwa Katika Shura

Mwongozo ufuatao ulitolewa na Khalifatul Masih II, Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmuud Ahmad r.a. kwa ajili ya Wajumbe wa Shura.

1. Hatukuja hapa kwa manufaa yoyote ya kidunia. Mimi naishi Qadian na wala sikutoka nje lakini baadhi yenu ni wakulima na hivyo imebidi kuacha mashamba yenu jambo ambalo ni gumu sana. Baadhi yenu ni wafanya biashara na baadhi yenu mmeajiriwa na bila shaka mlikuwa na mambo mengi ya kufanya lakini mliyaacha ili mje hapa. Hivyo tukumbuke tuko hapa kwa ajili ya Allah na tumtegemee Yeye tu. Jambo hili ni muhimu zaidi kwa sababu sisi tunapambana na dunia yote na tunapambana na watu wenye uzoefu mkubwa na wenye uwezo, wanadhibiti majeshi na serikali wakati sisi tumeazimia kuitawala dunia ilhali hatuna nguvu wala rasilimali wala uzoefu wala ujuzi na kwa hakika ni dhaifu katika kila nyanja. Katika hali hii mashauriano yetu yanaweza kuzaa matunda tu ikiwa tutamkimbilia Mwenyezi Mungu. Ushauri wangu wa kwanza kwenu ni kumuomba Mwenyezi Mungu na kulia kwa ajili ya msaada Wake. Mnatakiwa muombe hivi: ***"E Allah nimekuja hapa kwa ajili yako, Niongoze ili jambo lolote la kibinafsi lisipenye katika mawazo yangu na wala nisitoe ushauri potofu na kusisitiza juu yake na kwa kufanya hivyo kuidhuru imani, wala nisishawishike kukubali maoni ya mtu mwingine yasiyokuwa sawasawa kwa sababu tu ya umahiri wake wa kuzungumza. Nakuomba pia ile nafsi ya umimi isijitokeze na dhamira ya umaarufu na heshima visiingie akilini mwangu wala nisiwe na majivuno au kutoa ushauri mbaya na wenye kudhuru, wala kuukubali ushauri mbaya. Naomba dhamira yangu ielekee kwenye mambo safi na ushauri wangu uwe sahihi ambao uko chini ya mapenzi Yako".*** Kila mtu aombe namna hii, sio leo tu, bali wakati wowote wa mashauriano ya Jamaat.

2. Ushauri wa kwanza ni maombi, lakini hakuna maombi yanayokubaliwa mpaka yaambatane na vitendo. Kwa mathalan mtu anaweza kuomba apewe uwezo wa kuitumikia dini lakini kama hayuko tayari kutoa hata senti tano, kwa ajili hiyo atawezaje kutoa huduma yoyote? Maombi lazima yafuatane na vitendo. Hivyo nawaambieni wekeni kando fikra zote za ubinafsi. Leo, kesho na wakati wowote ambao Shura inakutana. Watu wengine wanakuja na mawazo yao tayari ambayo wanataka yakubalike. Lakini jambo hili haliendani na Shura. La msingi ni kuwa huru kifikira na kusema lililo sahihi. Watu wengine wanakuja hapa wakiwa wameamua tayari kwamba wazo lao lazima likubaliwe na wanafanya kila njia kuhakikisha kwamba hili linafanyika. Lakini huu si mwenendo wa Jamaat yetu. Sisi tunatakiwa tuseme na kusisitiza juu ya kile kilichokuwa sahihi.

3. Tunapokaa kwenye Shura lazima tuwe tayari kukubali wazo zuri na sio kusistiza juu wazo letu tu.

4. Jambo jingine ambalo ni muhimu kukumbuka sasa hivi na wakati wote wa Shura ni kwamba mtu asitoe wazo kwa ajili ya mtu fulani. Wapo watu wengine ambao hutoa wazo lakini baadae husema kwamba wazo hilo halikuwa lao isipokuwa rafiki yao aliwaambia walieleze jambo hilo. Tabia hii ni hatari sana, lakini la ajabu ni kwamba jambo hili halizingatiwi. Na ajabu zaidi ni kwamba hata wale waliobobea katika uongozi hutenda kosa hili. Mjumbe mmoja wa Kansel huko India aliwahi kusema ya kwamba wazo alilolitoa halikuwa lake. Waahmadiyya wajiepushe na tabia hiyo. Wasitoe wazo kwa niaba ya mtu mwingine, bali waseme tu kile wanachokielewa wao wenyewe kuwa ni sahihi.

5. Dhamira peke yake iwe ni kutoa ushauri wenye faida kuhusu mada husika. Ngoja nitoe mfano wakati wa mjadala iwapo mradi mpya uanze au usianze, watu wengine ingawaje wanaelewa umuhimu wa mradi huo wanaupinga kwa sababu tu wanaelewa fulani atachaguliwa kuuongoza. Mara nyingine wanafanya hivyo kwa nia mbaya kabisa na mara nyingine hawafikirii kuwa mtu huyo anafaa kwa ajili ya kazi hiyo. Badala ya kueleza kuwa aliyechaguliwa kuongoza mradi hafai wanapinga mradi mzima, hilo ni jambo baya na Wanajumuiyya wanatakiwa wajiepushe nalo.

6. Tusisite kuyakubali mawazo sahihi kutoka kwa yeyote yule. Yeyote apingae wazo sahihi kwa sababu tu limetolewa na mtu anayepingana naye, huyo anafanya kosa la kutokuwa mwaminifu.

7. Usikubali mawazo ya mtu mwingine kwa papara. Baadhi ya watu hawana wazo lao wenyewe,

Endelea uk. 11